
Vodacom Tanzania Public Limited Company

Taarifa ya Pamoja ya mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2025

Vodacom Tanzania Public Limited Company

# Taarifa ya Pamoja ya mwaka

ulioishia tarehe 31 Machi 2025



Pamoja tunaweza



# Yaliyomo

## Utangulizi

02 Sisi ni nani
03 Mahali huduma zetu zinapopatikana
04 Huduma na bidhaa zetu
05 Thamani tuliyoijenga


## Utawala

08 Taarifa ya Mwenyekiti
10 Viongozi wetu
Muundo wa Bodi
12 Kamati ya Utendaji
14 Taarifa ya uongozi wa kampuni
16 Taarifa ya shughuli za uongozi
18 Utaratibu wetu wa Ujira


## Biashara yetu

20 Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji


## Utendaji wa azma yetu

24 Kuiwezesha jamii
27 Kulinda sayari
29 Kuendeleza uaminifu


## Ufanisi wetu kifedha

32 Taarifa ya Mkurugenzi wa Fedha


## Taarifa ya mkutano mkuu

41 Taarifa ya mkutano mkuu
45 Fomu ya mwakilishi
46 Maelekezo ya fomu ya mwakilishi


## Taarifa za ziada

47 Taarifa kuhusu umiliki
48 Taarifa za kampuni
49 Dai la haki


**Ili kupata taarifa zaidi:**

UK Soma taarifa hii kwa kina

Soma zaidi katika tovuti www.vodacom.co.tz

## Maelezo ya msingi

Tafadhali zingatia kwamba, hii ni tafsiri ya taarifa ya mwaka kwa ufupi. Taarifa kamili ya mwaka imetolewa kwa lugha ya kiingereza. Iwapo utatokea mkanganyiko wa tafsiri, taarifa ya kiingereza itatumika.

Thamani iliyojengwa | Thamani iliyopungua | Thamani endelevu

# **Kuhusu** taarifa hii

Tunajivunia kuwasilisha Taarifa ya Pamoja ya Vodacom Tanzania, inayoonesha jinsi azma yetu ya kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora – inavyoongoza mkakati wetu na kuchangia ukuaji wa uchumi nchini Tanzania. Taarifa hii pia inatoa mtazamo wa kina kuhusu matarajio ya Kampuni katika siku za usoni na kuelezea kwa nini tunaamini kuwa Vodacom Tanzania inatoa fursa na kuvutia kwa uwekezaji wa muda mrefu.

### Mipaka na wigo wa taarifa hii

Taarifa hii inatoa maelezo ya kiutendaji ya Vodacom Tanzania Plc na kampuni zake tanzu kwa mwaka wa fedha ulioanzia 1 Aprili 2024 hadi 31 Machi 2025. Taarifa hii inawalenga wawekezaji wa sasa na wa siku zijazo, na inatoa muhtasari wa muundo wa biashara yetu na mazingira ya uendeshaji, na pia, inapitia utendaji wetu wa kimkakati, mfumo wa uendeshaji na wa utawala. Taarifa hii inajumuisha mambo yote ambayo tunaamini yanaweza kuchangia katika tathmini ya wasomaji, kuhusu thamani na matarajio ya utendaji wa kampuni kifedha katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

### Mifumo na utaratibu wa utoaji wa taarifa hii

Utaratibu wetu wa kutoa taarifa ya mwaka umekuwa ukiongozwa na kanuni na masharti yaliyo katika Viwango vya Kimataifa vya Taarifa za Fedha (IFRS), Kanuni za Soko la Hisa la Dar es Salaam za mwaka 2022 na Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Mkaguzi huru, Ernst & Young ('EY') amethibitisha taarifa zetu za fedha za mwaka na kutoa hati safi. (ukurasa wa 89 hadi 91 kwenye nakala ya kiingereza).

### Mfumo wetu wa utoaji taarifa

Mfumo wetu wa utoaji wa taarifa unalenga kukidhi mahitaji mbalimbali ya wadau wa Kampuni yetu, ukiwawezesha kutathmini utendaji wetu wa kifedha na usio wa kifedha.

### Taarifa za matarajio ya baadaye

Matarajio yetu ya baadaye yaliyoanishwa katika taarifa hii ni pamoja na changamoto tunazoweza kukumbana nazo na fursa tunazokusudia kuzifanyia kazi kama sehemu ya mkakati wetu. Na pia jinsi hatua hizi zinavyoweza kuathiri utendaji wetu. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa taarifa za matarajio ni za matukio na hali ambazo zinaweza kutokea au kutokutokea.

### Azma yetu kuu ya kuongeza thamani katika jamii

Vodacom Tanzania imejikita katika kuboresha maisha ya mamilioni ya Watanzania kupitia azma yetu ya **kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora.** Tunatambua kuwa ili kutimiza azma hii, masuala ya mazingira, jamii na utawala ni muhimu kuzingatiwa katika utendaji wetu ikilenga:

- Kuiwezesha jamii (EP)
- Kulinda sayari (PP)
- Kuendeleza uaminifu (MT)

Taarifa hii inajumuisha mchango wetu katika masuala ya mazingira, jamii na utawala.

UK Soma zaidi kuhusu utendaji wetu unaoongozwa na azma yetu ukurasa wa 24 hadi 31

Soma zaidi kuhusu mchango wetu katika jamii kupitia azma yetu katika tovuti yetu www.vodacom.co.tz

**TAARIFA HII**

**Taarifa ya Pamoja ya Mwaka**

Taarifa yetu ya Pamoja ya Mwaka ni nyenzo kuu ya mawasiliano na wadau wetu, ikikamilishwa na taarifa za ziada kulingana na mfumo wetu wa utoaji taarifa.

**Taarifa ya masuala ya mazingira, jamii na utawala (ESG)**

Taarifa yetu ya masuala ya mazingira, jamii na utawala inalenga kukidhi mahitaji ya taarifa mbalimbali kwa wadau wetu na kutoa muhtasari wa jinsi tunavyoiwezesha jamii, kulinda sayari na kuendeleza uaminifu.

**Taarifa za ziada kifedha na taarifa za wahanisa wetu**

Tunatoa taarifa za kina kuhusu ufanisi na utendaji wetu kifedha kupitia taarifa zetu za kifedha za mwaka. Pia, tunawapatia wanahisa wetu taarifa muhimu kwa ajili ya ushiriki wao kamilifu katika mkutano wetu mkuu wa mwaka kupitia taarifa yetu ya mkutano mkuu.

### Ushiriki wa Bodi katika uandaaji wa Taarifa hii

Bodi imeshiriki kikamilifu katika uandaaji na uwasilishaji wa taarifa hii. Na tunaamini kuwa taarifa hii inaelezea masuala yote muhimu, na inawasilisha maelezo yenye usahihi kuhusu utendaji wa kundi la Makampuni kwa kipindi husika na vilevile inatoa taswira halisi ya mikakati yetu ya utekelezaji. Wakurugenzi wanaamini kuwa kutangaza mipango mkakati ya Vodacom Tanzania, hakutaleta athari yeyote ile katika medani za ushindani wa kibiashara. Bodi ilipitisha taarifa hii ya mwaka tarehe 15 Julai 2025.

D Tarimo, Mwenyekiti
P Besiimire, Mkurugenzi Mtendaji
H Bujiku, Mkurugenzi wa Fedha

Wakurugenzi huru
K Mutooni
M Ikongo
T Semane

Wakurugenzi wasio watendaji
M Abdallah
D Kastelic
H Ammar
M Mbungela
N Nyoka
R Morathi

# **Sisi** ni nani

Vodacom Tanzania ni kampuni inayoongoza nchini Tanzania kwa kutoa huduma za mawasiliano kwa wateja wa matumizi binafsi na biashara ikiwa ni pamoja na huduma za simu sauti, data, ujumbe mfupi wa Maneno na huduma za fedha kwa wateja zaidi ya **milioni 22.6[1]**.

Vodacom Tanzania iliorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam mnamo Agosti 15, 2017. Mmiliki mkubwa wa Vodacom Tanzania na kampuni zake tanzu (yaani 'Kundi la Kampuni za Vodacom') ni Vodacom Group Limited, kampuni iliyosajiliwa Afrika Kusini ambayo nayo inamilikiwa na Vodafone Group Plc ya Uingereza.

**Azma yetu**
Kwanini tupo

Kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora

**Nguzo kuu za azma yetu**

**Kuiwezesha jamii**
Tunakusudia kupunguza ombwe la kidigitali na kuwezesha watu wengi kunufaika na maisha Jumuishi ya kidigitali

**Kuilinda sayari**
Tunakusudia kulinda sayari kwa kupunguza athari za mazingira na pia kuwawezesha wateja wetu kufanya vivyo hivyo

**Kuendeleza uaminifu**
Tunakusudia kuendelea kuendesha biashara kwa misingi ya uwajibikaji.

**Dira yetu**
Tunakoelekea na tunataka kuwa nani

Kuwa **kampuni ya kidigitali inayoongoza** ambayo inawezesha jamii iliyounganishwa katika mtandao

Kuwa **mwajiri bora** (mahali bora pa kufanyia kazi)

**Kwa namna gani**
Namna ya utekelezaji

1. **Kuaminiwa na wateja**
2. **Kujenga mustakabali**
3. **Kufanya majaribio – kujifunza haraka**
4. **Kutekeleza mambo yote kwa pamoja**

**Vipaumbele vyetu kimkakati**

**Ukuaji kupitia biashara mpya huku tukilinda biashara zetu kuu**


- Kulinda kwa bidi biashara ya **huduma ya mawasiliano ya simu**
- Kuongeza wigo na **kuikuza huduma ya M-Pesa**
- Kuzifikia **fursa za kutoa huduma ya data majumbani na maofisini**
- Ubunifu na kuongoza katika **huduma kwa wateja wa kibiashara**
- **Kukodisha sehemu ya rasilimali zetu**
- **Thamani ya chapa yetu** katika soko

Udigitishaji wa huduma kwa wateja | Uongozi katika teknolojia ya mtandao na **TEHAMA** | Kuwaendeleza wafanyakazi na kuwa na timu ya watu wanaofanya kazi kwa ufanisi

Kuongeza **ufanisi wa matumizi ya mtaji**

1 Katika taarifa hii, popote itakapozungumziwa idadi ya wateja, itakuwa ni idadi ya wateja kwa kadiri ya kanuni za tafsiri ya mteja za kundi la makampuni ya Vodacom.

# **Mahali** huduma zetu zinapopatikana




| Minara ya 5G | Minara ya 4G | Minara ya 3G | Minara ya 2G |
|---|---|---|---|
| 370 | 3 275 | 3 554 | 3 704 |

**Uwekezaji wetu** (Shilingi bilioni)

| | |
|---|---|
| MACHI-22 | 174 |
| MACHI-23 | 156 |
| MACHI-24 | 170 |
| MACHI-25 | 175 |

**Wateja wa siku 90** (milioni)[2]

| | |
|---|---|
| MACHI-22 | 15.4 |
| MACHI-23 | 16.7 |
| MACHI-24 | 19.6 |
| MACHI-25 | 22.6 |

**Idadi ya watu wanaofikiwa na mtandao wetu wa 3G na 4G[1]**

| | |
|---|---|
| MACHI-22 | 65.8% |
| MACHI-23 | 66.9% |
| MACHI-24 | 72.0% |
| MACHI-25 | 69.4% |

**Idadi ya minara**

| | |
|---|---|
| MACHI-22 | 3 388 |
| MACHI-23 | 3 447 |
| MACHI-24 | 3 481 |
| MACHI-25 | 3 704 |

**Idadi ya minara ya 4G**

| | |
|---|---|
| MACHI-22 | 1 963 |
| MACHI-23 | 2 353 |
| MACHI-24 | 2 804 |
| MACHI-25 | 3 275 |

**Idadi ya watu wanaofikiwa na mtandao wetu wa 4G1[1]**

| | |
|---|---|
| MACHI-22 | 50.4% |
| MACHI-23 | 56.2% |
| MACHI-24 | 66.1% |
| MACHI-25 | 72.5% |

1 Imepimwa katika kiwango cha 1 mbps (nje).
2 Idadi kadiri ya kanuni za kundi la makampuni ya Vodacom.

# **Huduma** na bidhaa zetu

Tuna wateja zaidi ya **milioni 22.6** wanaotumia bidhaa na huduma zetu.

## Huduma kwa matumizi ya wateja binafsi na kidigitali

**Sauti**
- Simu za kiganjani

**Data**
- Modemu za broadband
- Intaneti kwa simu
- Intaneti ya majumbani na maofisini

**Ujumbe mfupi**
- Ujumbe mfupi wa maneno na programu za mitandao ya kijamii

**Huduma za ziada**
- Vyombo vya habari na burudani (habari, video na miziki ya kidigitali na michezo ya bahati nasibu)
- Elimu na matangazo (Silabu na SmartBango)
- Huduma binafsi (tovuti yetu na Nipige tafu)
- Afya (Afyacall na Elimika)

**Huduma kwa wateja**
- Kituo cha mawasiliano
- Dawati la huduma kwa wateja
- Maduka ya Vodacom
- Huduma binafsi (USSD code, M-Pesa app)
- Huduma za kidigitali (kupitia mitandao ya kijamii, tovuti, Whatsapp na Live Chat app) Viashiria kwa wateja (ujumbe ibukizi)
- Huduma jumuishi na kaunta maalum kwa wateja wenye mahitaji maalum

## M-Pesa

**Kuweka na kutoa fedha**
- Kwa mawakala zaidi ya 225 000

**Kuhamisha na kupokea fedha kati ya wateja wetu**
- Kutuma pesa ndani ya nchi na kimataifa (IMT)

**Huduma binafsi**
- Aplikesheni ya M-Pesa

**Mifumo ya malipo ya kielektroniki**
- Kadi za kielektroniki 'M-Pesa Visacard'
- Mfumo wa malipo wa 'Lipa kwa Simu'
- Mteja kwenda kwenye Biashara 'C2B'
- Biashara kwenda kwa Mteja 'B2C'
- Biashara kwenda kwa Biashara 'B2B'

**Huduma za kifedha**
- Huduma ya mikopo ya Songesha
- Akiba na mikopo (M-Pawa, M-Godi)
- Akaunti za akiba za vikundi (M-Koba na Changisha)
- Mikopo ya muda mrefu ya mawakala
- Huduma za bima
- Uwekezaji (M-Wekeza)

## Matumizi ya wateja wa Biashara

**Simu za kiganjani**
- Sauti
- Vifurushi kwa wateja wadogo wa kibiashara
- Data
- Intaneti ya Vitu
- Ujumbe mfupi wa maneno Huduma binafsi
- Huduma za ziada

**Huduma za data majumbani na maofisini na ukodishaji wa sehemu za rasilimali zetu**
- Huduma za intaneti
- Unganishaji wa kampuni na matawi yake
- Huduma za ukodishaji
- Huduma za uhifadhi wa rekodi kielektroniki
- Mkongo maalum kwa ajili ya makampuni
- Huduma za kidigitali kama M-Kulima
- M-Pesa kwa biashara (akaunti za makusanyo na malipo)

# **Thamani** tuliyoijenga

## Thamani tuliyoijenga kwa mwaka wa fedha 2025

Wateja
milioni **22.6**
Ongezeko la 15.7%

Wateja wa M-Pesa
Ongezeko la **13.3%**

Wateja wa data
Ongezeko la **19.0%**

Watumiaji wa simu janja
Ongezeko la **33.4%**

Mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu (EBITDA)
Shilingi bilioni **493.6**
Ongezeko la 25.2%

Mapato ya huduma
Shilingi trilioni **1.5**
Ongezeko la 20.5%

Mapato ya M-Pesa
Shilingi bilioni **590.0**
Ongezeko la 29.3%

Mapato ya data
Shilingi bilioni **422.2**
Ongezeko la 21.6%

Faida baada ya kodi
Shilingi bilioni **90.5**
Ongezeko la 69.4%

Gharama ya uwekezaji
Shilingi bilioni **175.0**
Ongezeko la 2.9%

**11.4%** ya mapato

Minara mipya
**471**
ya 4G



## Kwa wateja wetu

Huduma za **mawasiliano zilizoboreshwa**

Kutanua wigo wa ujumuishi kifedha kupitia **M-Pesa**

Fursa ya kuweweka na kuingiza kipato kupitia **M-Wekeza**

Huduma za kuaminika – zikithibitishwa na uongozi wetu katika kipimo cha kuridhika kwa wateja (NPS)

### Ongezeko la ujumuishi kidigitali kupitia uwekezaji wetu endelevu katika mtandao

4G — Wigo wa teknolojia ya 4G[1] **72.5%** ya idadi ya watu ongezeko la 6.1%

3G — Wigo wa teknolojia ya 3G **86.7%** ya idadi ya watu imepungua kwa 5.3%

2G — Wigo wa teknolojia ya 2G **95.1%** ya idadi ya watu ongezeko la 1.1%

1 Imepimwa katika kiwango cha Mbps 1 (nje).



## Kwa wanahisa wetu

**Shilingi bilioni 45.3**
gawio linalopendekezwa kwa wanahisa

Ongezeko la faida katika biashara

## Kwa wafanyakazi wetu

**Shilingi bilioni 90**
zimetumika kwa wafanyakazi, ikiwemo kwenye mishahara, mafunzo na kuendeleza ujuzi

**Mwaka wa fedha 2024:** Shilingi bilioni 75

Tumetoa mafunzo ya kujiendeleza kupitia mtandao kwa zaidi ya wafanyakazi
**624**

**Mwaka wa fedha 2024:** 607

**47.1%**
uwakilishi wa wanawake kwenye uongozi wa Kampuni

**Mwaka wa fedha 2024:** 46.7%

## Katika jamii yetu

Tumechangia jumla ya
**Shilingi bilioni 621**
katika fedha za umma kwa njia ya kodi, tozo, masafa na tozo za mamlaka za udhibiti wa sekta[1]

**Minara 422**
imejengwa tangu mwaka 2013 katika kuunga mkono juhudu za serikali za kufikisha mawasiliano vijijini


**Shilingi bilioni 717.3**
zimetumika kwa ajili ya malipo ya bidhaa na huduma za wasambazaji wa ndani na makampuni washirika 327 nchini Tanzania

Takriban
**Shilingi bilioni 3.7**
zimetumika katika uwekezaji kwenye jamii[2]

Ajira zisizo za moja kwa moja zimetolewa kwa zaidi ya Watanzania
**250 000**[3]

Uwezeshaji wa kijamii na kiuchumi kupitia mikakati mbalimbali katika utekelezaji wa azma yetu

1 Maelezo ya ziada yanapatikana katika Taarifa ya masuala ya kodi ya Kampuni yetu Mama ya Vodacom inayopatikana kupitia https://www.vodacom.com/integrated-reports.php.
2 Inajumuisha ufadhili wa fedha na thamani ya vifaa au vitu vilivyotolewa kupitia matukio mbalimbali ya Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR).
3 Inajumuisha wafanyabiashara wadogo huria (Freelancers) na mawakala wa M-Pesa.





# Taarifa ya Mwenyekiti

**Jaji (mstaafu) Thomas B Mihayo**

Mwaka huu, Vodacom Tanzania imefanikiwa tena kupata matokeo mazuri kiutendaji yanayoakisi azma yake, yakichagizwa na matokeo thabiti ya kifedha na kiutendaji kutokana na utekelezaji bora wa mkakati wake. Inafurahisha kwamba Vodacom ilipata ongezeko la 69.4% kwenye faida baada ya kodi hadi kufikia shilingi bilioni 90.5. Matokeo haya yanaiwezesha Bodi kupendekeza gawio la 50% ya faida baada ya kodi, kulingana na sera yetu ya gawio.

Katika mwaka uliopita tulishuhudia changamoto mbalimbali ikiwemo mivutano ya kisiasa duniani, kuvurugika kwa minyororo ya usambazaji bidhaa na kuongezeka kwa vita vya kibiashara. Pia matukio ya hali mbaya ya hewa, kama vile mafuriko na ukame ambayo yaliathiri uchumi na watu. Kwa bahati nzuri mazingira imara na rafiki kibiashara hapa nchini kwetuTanzania, yalisaidia kupunguza athari ya baadhi ya changamoto hizi. Tulitiwa moyo sana na **hali ya uendelevu wa uthabiti wa taratibu za usimamizi wa ki-sekta na ushirikiano mzuri wa serikali** katika kutatua changamoto zilizoathiri sekta ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na hivyo kuendeleza ukuaji wa uchumi jumuishi unaowezeshwa na uunganishaji wa kidigitali.

Uthabiti wetu katika ksuimamia azma yetu ya kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora, uliendelea kuwa kigezo muhimu cha kututofautisha katika soko hili lenye ushindani mkubwa, hasa kutokana na matarajio makubwa na yanayobadilika badilika ya wateja wetu. Katika mazingira haya, ilikua ni jambo la kutia moyo sana kuona kampuni ikitekeleza mikakati yake kwa uthabiti bila kutetereka. Utendaji huu uliwezesha ongezeko la idadi ya wateja wetu kwa 15.7%, na kuendeleza uongozi wetu katika soko tukiwa na 31.9%[1] ya wateja wote.

Kwa kiasi kikubwa, **lengo letu la kuiwezesha jamii kupitia udigitishaji limeendelea kupiga hatua kubwa.** Tumepanua wigo wa mtandao wetu wa data, tumeunganisha huduma ya mawasiliano katika maeneo yaliyokosa huduma hii hapo awali, tumetekeleza jitihada muhimu za kuongeza kasi ya kusambaza simu janja na kuboresha zaidi huduma zetu za data kwa simu. Juhudi hizi zilisaidia ongezeko la matumizi ya data, hususan kupitia teknolojia ya 4G.

Pia kupitia M-Pesa, tumewezesha ongezeko la ushirikishwaji kifedha hasa kwa watu wasiotumia huduma za benki.. Mwaka huu, karibu nusu ya wateja wa M-Pesa wametumia huduma zetu za kisasa za fedha, ikiwemo kukopa, kuweka akiba na kukata bima, wakinufaika na huduma mbalimbali za mikopo ya muda mfupi, ikiwa ni pamoja na Songesha na mikopo mingine ya muda mfupi. Huduma hizi za kifedha zimekuwa nyenzo muhimu katika kuwawezesha wateja wetu, kuimarisha jamii na kuongeza mafanikio yetu ya kibiashara.

Zaidi ya hayo, **utamaduni thabiti wa kimaadili na utawala bora** umeendelea kuwa msingi imara wa utekelezaji wa azma yetu. Kama Mwenyekiti, nilikuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba Bodi, kupitia kamati zake, inaweka dira inayoongoza juhudi za uongozi wa kampuni katika kufanikisha maendeleo endelevu na matokeo chanya kifedha kwa faida ya wadau wetu. Tathmini yetu huru ya hivi karibuni kuhusu utendaji wa Bodi, ilinithibitishia kuwa katika tuna mlingano na muundo sahihi wa kutuwezesha kusimamia kwa uthabiti malengo ya kimkakati ya kampuni. Pia, ilinifurahisha kuona Kamati ya Utendaji chini ya usimamizi wa Bodi, inatekeleza mikakati iliyowezesha mafanikio kiutendaji kwa manufaa ya wanahisa na taifa kwa ujumla, sambamba na azma yetu.

**Mwisho wa mwaka huu wa fedha, baada ya miaka mitano ya utumishi katika Bodi, nilijiuzulu kutoka nafasi yangu ya Mwenyekiti.** Ninapotafakari kipindi changu cha uongozi, ninajawa

1 Kwa mujibu wa takwimu za mawasiliano za robo mwaka za Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania za Machi 31, 2025.





na hisia kubwa za shukrani na fahari, kwa kuwa sehemu ya kampuni hii yenye vipaji na mtazamo chanya wa kubadili maisha ya baadaye.

Nimeridhishwa sana na mafanikio tuliyopata katika **utekelezaji wa azma ya kampuni katika miaka hiyo mitano.** Nitataja mifano michache tu.

Miongoni mwa mipango ninayoipenda sana kwa kuwa ina matokeo makubwa ni M-Mama. Mpango huu umesaidia kuokoa maisha ya akina mama wajawazito na watoto wachanga katika maeneo ambayo usafiri wa magari ya dharura haupatikani. M-Mama, iliyozinduliwa kwa ushirikiano na washirika wetu – serikali ya Tanzania na USAID, inarahisisha usafirishaji wa wajawazito waliorodheshwa katika mpango huu, wanapokwenda katika vituo vya afya kwa kutumia teksi za kawaida, zinazoendeshwa na madereva waliofunzwa na kusajiliwa kwenye mfumo wa M-Mama. M-Mama inatoa mchango muhimu katika kupunguza vifo vya kina mama wajawazito.

Katika kipindi changu cha uongozi, pia tulifanikiwa kuunganisha mamilioni ya Watanzania kwa kesho iliyo bora kupitia maboresho na upanuzi wa wigo wa mtandao wetu na kuwafikia wateja wengi zaidi. Tumepanua wigo wa mtandao wetu wa 2G kutoka asilimia 89.8% hadi kufikia asilimia 95.1% ya idadi ya watu, na wigo wa upatikanaji wa mtandao wetu wa data[1] hadi kufikia asilimia 69.4% kutoka asilimia 49.2% ya kipindi cha mwaka wa fedha 2020. Idadi ya watu waliofikiwa na mtandao wetu wa teknolojia ya 4G saas imefikia 72.5% ikitoka asilimia 32.6% katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020. Kwa namna ile ile tulivyo ongeza wigo wa mtandao wetu, tuliendeleza pia upatikanaji wa huduma bora za data kwa Watanzania, kwa kuongeza idadi ya watumiaji wa simu janja kutoka chini ya milioni nne, hadi kufikia karibu milioni tisa. Hatua hii inawawezesha wateja wetu kuzifikia fursa mbalimbali katika uchumi wa kidijitali.

Mafanikio tunayojivunia zaidi ni uzinduzi wa **mtandao wa kwanza kabisa wa teknolojia ya 5G nchini Tanzania.** Hii si tu kwamba ni hatua kubwa kiteknolojia, bali wakati muhimu unaodhihirisha dhamira yetu thabiti ya maendeleo, ubora, na mustakabali wa siku zijazo.

Mafanikio mengine ya kukumbukwa ni mageuzi na kukua kwa huduma yetu ya M-Pesa, inayosaidia kuwawezesha Watanzania kushirikishwa kifedha. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, zaidi ya shilingi trilioni 400 zimechakatwa kupitia M-Pesa, na kubadilisha maisha ya mamilioni ya watu, si tu kupitia huduma za msingi kama kutuma na kupokea pesa, bali pia kupitia huduma mbalimbali zenye utofauti na za kimageuzi kama mikopo ya Songesha, mikopo ya muda mfupi, huduma za bima, akiba za vikundi kupitia M-Koba, na huduma mpya ya M-Wekeza, inayowezesha uwekezaji katika rasilimali za kifedha kupitia wasimamizi wa mifuko ya uwekezaji.

M-Pesa pia imebadilisha namna Watanzania wanavyofanya malipo, kwa kuwezesha malipo ya kidigitali kupitia mtandao wa wafanyabiashara zaidi ya 470 000 wanaopokea malipo kupitia huduma yetu ya LIPA kwa Simu, pamoja na akaunti zaidi ya 800 za makusanyo ya serikali zilizopo kwenye mfumo wa M-Pesa, ambazo hurahisisha mchakato wa malipo kwenda serikalini.

**Katika kuchangia ukuaji wa biashara,** najivunia sana kuhusika katika kuimarisha majadiliano ya wazi na yenye tija kati ya kampuni, wadau wa biashara, wadhibiti wa sekta na serikali – mazungumzo ambayo yamechangia kuleta mabadiliko ya kweli katika nchi yetu.

**Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali na idara zake,** hasa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Wizara ya Fedha, pamoja na wadhibiti wetu – Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA). Kwa kiwango kilekile, **ningependa pia kutambua na kuishukuru ofisi ya Spika wa Bunge la Tanzania,** kwa ushirikiano mkubwa tulioupata kutoka kwa Bunge na kamati zake mbalimbali ambazo tulifanya nazo kazi mara kwa mara wakati wa kipindi changu cha uongozi.

Serikali na Bunge zilionesha utayari wa kusikiliza hoja zetu na kwa pamoja tukatatua masuala kadhaa. Mfano mzuri ni kupunguzwa kwa tozo katika miamala ya huduma za kifedha kwa simu ambao zilianza Julai 2021. Jambo hili ni kati ya mengine mengi, ambayo tuliuomba Uongozi wa nchi kuyaangalia upya, kwa maendeleo ya sekta yetu na kuimarisha mchango wa sekta katika kupunguza ombwe la kijigitali na kukuza ushirikishwaji kifedha.

Utayari wa Serikali na Bunge kushirikiana na wawekezaji na wadau wa sekta binafsi, ni mfano wa kuigwa wa uongozi bora, na dhamira ya kuendeleza sekta na nchi kwa ujumla.

Juhudi na mipango hii ilichangia katika utendaji mzuri wa kampuni, na kuirejesha katika kuzalisha faida baada ya miaka michache ya awali iliyokuwa na changamoto ya Uenyekiti wangu. Ninashukuru na ninaona fahari sana kwa miongozo ambayo Bodi yangu ilitoa kwa timu ya utendaji, ambayo ilisaidia kuirejesha biashara kwenye kuzalisha faida na kuongeza manufaa kwa wanahisa.

**Tukingalia siku zijazo,** tunatambua uwezekano wa kutokea changamoto zitokanazo na mazingira ya kibiashara katika uchumi wa dunia uliounganika na wenye muingiliano mkubwa. Hata hivyo, nina matumaini makubwa juu ya uimara na hali ya kiuchumi na kijamii nchini Tanzania. Mwezi Oktoba 2025, tunatarajia kuwa na uchaguzi mkuu wa Rais na wabunge, ambao naamini utakuwa wa amani. Muhimu zaidi ya yote, nina uhakika kwamba kampuni inaendeshwa katika mtazamo sahihi wa ukuaji, unaoweza kukabiliana na hali ya sintofahamu na kuimarisha nafasi yake ya mtoa huduma wa mawasiliano kwa simu anayeongoza nchini Tanzania.

Kwa kumalizia, ningependa kuwashukuru wenzangu katika Bodi na kamati mbalimbali za Bodi kwa msaada wao wa thamani,mang'amuzi, maarifa, ushauri na kujitoa kwao katika kuimarisha viwango vya juu vya utawala bora. Ningependa pia kumshukuru Katibu wetu wa Kampuni kwa mwongozo wa utaalamu wake. Imekuwa heshima kubwa kuhudumu kama Mwenyekiti wenu.

Shukrani zangu za dhati ziende kwa Mwenyekiti wa Bodi na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni yetu mama ya Vodacom Group, pamoja na timu ya uongozi ya Vodacom Tanzania. Kipekee nimshukuru kila mmoja wa Wakurugenzi Watendaji walioongoza kampuni wakati wa kipindi changu cha uongozi. Katika kipindi chote cha miaka mitano, nimekuwa nikivutiwa na kina cha maarifa na jitihada zilizooneshwa na timu ya uongozi wa kampuni pamoja na wafanyakazi.

Ninaamini Vodacom Tanzania ni kampuni yenye uwezo wa kufanya mambo makubwa zaidi. Ninawahimiza wadau wetu wote kuendelea kuihamasisha kampuni hii, ili tuweze kuunganisha Watanzania kwa kesho iliyo bora na kubadili maisha yao kupitia teknolojia.

Ninapowaaga, ninapenda kumkaribisha mrithi wangu, Mwenyekiti mpya Bwana David Tarimo. Ninamtakia kila la heri katika kuendeleza kampuni hii kubwa yenye malengo thabiti.

**Jaji (mstaafu) Thomas B Mihayo**
Mwenyekiti
31 Machi 2025

1 MKipimo kwa Mbps 1.

# Viongozi wetu

## Muundo wa Bodi

Tuna Bodi yenye wakurugenzi 12, wengi wao ni wakurugenzi wasio watendaji. Mwenyekiti wetu ni mkurugenzi huru.

● Mwenyekiti
(A) Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji
(R) Kamati ya Ujira
(N) Kamati ya Uteuzi

### Mwenyekiti

**Thomas B Mihayo** (78)
*Mtanzania*
Aliteuliwa mwezi Novemba 2020*
- Utaalamu wa Sheria
- Msuluhishi
- Mahusiano na serikali



(N) Mwenyekiti

### Wakurugenzi watendaji

**Philip Besiimire** (49)
*Mganda*
Aliteuliwa mwezi Oktoba 2022
- Uongozi kimataifa na uzoefu katika uendeshaji wa biashara
- Utekelezaji wa mabadiliko ya kimkakati ya biashara
- Utekelezaji wa mikakati ya kibiashara akiwa na rekodi ya kipekee katika ukuzaji wa biashara



Mkurugenzi Mtendaji

**Hilda Bujiku** (46)
*Mtanzania*
Aliteuliwa mwezi Januari 2022
- Ujuzi mkubwa wa masuala ya fedha
- Uzoefu mpana katika masoko yanayoibukia



Mkurugenzi wa Fedha

* Thomas Mihayo alijiuzulu 31 Machi 2025.

### Wakurugenzi huru

**Kanini Mutooni** (49)
*Mkenya*
Aliteuliwa mwezi September 2022
- Utaalamu wa fedha na mitaji ya ubia
- Mjumbe wa bodi mwenye uzoefu wa uongozi kimataifa



(A) (R) (N)

**Margaret Ikongo** (67)
*Mtanzania*
Aliteuliwa mwezi Novemba 2017
- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika
- Uzoefu katika utekelezaji wa shughuli za uendeshaji na mikakati
- Utaalamu wa fedha



(A)


**Thembeka Semane** (48)
*Mwafrika Kusini*
Aliteuliwa mwezi Novemba 2017
- Utaalamu wa fedha
- Mahusiano na serikali
- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika



(A)

### Wakurugenzi wasio watendaji

**Diego Gutierrez** (48)
*Mbolivia*
Aliteuliwa mwezi Machi 2018*
- Mpanga mikakati ya kibiashara
- Maarifa mapana kuhusu teknolojia ya simu na uzoefu wa masoko yanayoibukia
- Utaalamu wa uongozi wa kimkakati



(R)

**Nkateko Nyoka** (61)
*Mwafrika Kusini*
Aliteuliwa mwezi Aprili 2020
- Uzoefu katika sheria na sera za umma
- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika
- Uongozi na mahusiano na wadau



**Haytham Ammar** (43)
*Mmisri*
Aliteuliwa Juni 2024
- Uzoefu mkubwa katika mambo ya kifedha ndani ya sekta ya mawasiliano ya simu
- Utaalamu wa uongozi katika masuala ya kimkakati ya biashara



**Dejan Kastelic** (47)
*Mslovakia*
Aliteuliwa Aprili 2024
- Uzoefu mpana wa sekta ya mawasiliano na TEHAMA
- Uzoefu wa masoko mbalimbali ya kimataifa na yanayoibukia
- Utaalamu wa uendeshaji na utekelezaji wa mikakati



**Matimba Mbungela** (53)
*Mwafrika Kusini*
Aliteuliwa mwezi Agosti 2017
- Maarifa na uzoefu mpana wa usimamizi wa vipaji
- Utaalamu katika taratibu bora za kusimamia rasilimali watu
- Uzoefu katika uendeshaji wa shughuli za kimataifa



(R) (N)

**Raisibe Morathi** (55)
*Mwafrika Kusini*
Aliteuliwa mwezi Novemba 2020
- Uzoefu wa masuala ya fedha kimataifa
- Utaalamu wa uongozi kimkakati
- Utaalamu katika kung'amua fursa za kuunganisha au kununua biashara



* Diego Gutierrez alijiuzulu 1 Mei 2025.

### Katibu wa Kampuni

**Caroline Mduma** (47)
Aliteuliwa mwezi Aprili 2017
- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika



### Mgawanyo wa wajumbe wa Bodi

**Jinsia**

Wanawake **41.7%**

Wanaume **58.3%**


**Muundo wa Bodi**

Wajumbe 12

**2** Wakurugenzi watendaji

**6** Wakurugenzi wasio watendaji

**4** Wakurugenzi huru




Mahudhurio ya vikao vya bodi

**Umri**

| 35 – 39 | 40 – 49 | 50 – 59 | 60 – na zaidi |
|---|---|---|---|
| 0 | 7 | 2 | 3 |

**Muda waliohudumu kwenye nafasi hizi**

| Miaka 0-3 | Miaka 4-6 | Miaka 7-8 |
|---|---|---|
| 5 | 2 | 5 |

# Kamati ya Utendaji



**Philip Besiimire** (49)
Mkurugenzi Mtendaji
Alijiunga Vodacom mwaka 2022



**Hilda Bujiku** (46)
Mkurugenzi wa Fedha
Alijiunga Vodacom mwaka 2012



**Brigita Shirima** (46)
Mkurugenzi wa Biashara _ Wateja Binafsi
Alijiunga Vodacom mwaka 2012



**Epimack Mbeteni** (46)
Mkurugenzi wa Biashara – M-Pesa
Alijiunga Vodacom mwaka 2014



**Athumani Mlinga** (57)
Mkurugenzi TEHAMA
Alijiunga Vodacom mwaka 2003



**Andrew Lupembe** (51)
Mkurugenzi Masuala ya Mtandao
Alijiunga Vodacom mwaka 2007



**Olaf Mumburi** (48)
Mkurugenzi wa Sheria na Udhibiti
Alijiunga Vodacom mwaka 2008



**Zuweina Farah** (38)
Mkurugenzi wa Masuala ya Mahusiano na Taasisi ya Vodacom
Alijiunga Vodacom mwaka 2023



**Harriet Atweza Lwakatare** (47)
Mkurugenzi Huduma kwa Wateja
Alijiunga Vodacom mwaka 2012



**Vivienne Penessis** (49)
Mkurugenzi Rasilimali Watu
iunga Vodacom mwaka 2018



**Nguvu Kamando** (50)
Mkurugenzi wa Huduma za Kidigitali
Alijiunga Vodacom mwaka 2002



**Tax Agapinus** (60)
Mkurugenzi Dharura na Utekelezaji
Alijiunga Vodacom mwaka 2020

## Mgawanyo wa Kamati ya Utendaji

### Jinsia

Wanawake
**41.7%**

Wanaume
**58.3%**

### Umri

| 35 – 39 | 40 – 49 | 50 – 60 |
|---|---|---|
| 1 | 7 | 4 |

### Muda waliohudumu kwenye nafasi hizi

| Miaka 0-3 | Miaka 4-10 | Miaka 10+ |
|---|---|---|
| 2 | 2 | 8 |

### Utaifa

| Watanzania | Mganda |
|---|---|
| 11 | 1 |



# Taarifa ya uongozi wa kampuni

## Taarifa ya utekelezaji

Vodacom Tanzania Public Limited Company ('Vodacom Tanzania') inajizatiti kutoa huduma zenye ubora wa hali ya juu kwa uaminifu, maadili na utaalamu katika biashara.

Kanuni za uongozi wa kampuni zinajumuisha nidhamu, uhuru wa maamuzi, uwajibikaji, usawa, uwajibikaji kwa jamii, uwazi na uwajibikaji wa wakurugenzi kwa wadau. Kanuni hizi zinazingatiwa katika taratibu za udhibiti wa ndani na sera za Vodacom Tanzania zinazoongoza utendaji wa kampuni na zinawiana na miongozo ya Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana kuhusu taratibu za usimamizi wa shirika unaofanywa na kampuni za umma zilizoorodheshwa nchini Tanzania.

### Maadili ya viongozi

Bodi inakubali uwajibikaji wa pamoja katika kueleza namna ambavyo maadili na tabia za kimaadili zinapaswa kutekelezwa katika kampuni. Hii ni pamoja na kupanga taratibu za utendaji wa wajumbe wa bodi ili kuhakikisha kuwa wanatenda kwa uadilifu, uzoefu, uwajibikaji, haki na uwazi. Sifa hizi ni kipimo cha maadili kinachozingatiwa katika tamaduni za uendeshaji wa kampuni.

### Uongozi na Kamati za Bodi

**Bodi**

Vodacom Tanzania ina bodi yenye wakurugenzi 12, ambapo kati yao wanne (pamoja na Mwenyekiti) ni wakurugenzi huru wasio watendaji, sita kati yao si watendaji (lakini si huru kwa kuwa wanawakilisha wadau wakuu), na wawili ni wakurugenzi watendaji.

Bodi imeridhika kuwa uwiano wa wataalamu wenye maarifa, ujuzi na uzoefu wa aina mbalimbali ni wa kutosha.

Bodi inaweza kukutana kwa ajili ya kufanya shughuli, kuahirisha na vinginevyo kudhibiti mikutano yake itakavyoona inafaa. Mikutano ya bodi inafanyika mara kwa mara kupitia mkakati, ufanisi wa kiuendeshaji na kifedha, na vilevile usimamizi. Mikutano maalum ya bodi inaweza kufanyika wakati itakapohitajika.

Kamati ya Uteuzi hufanya mapitio ya utaratibu wa mwendelezo wa majukumu ya bodi na kamati zake ili kuhakikisha kuwa zina watu sahihi wenye ujuzi na uzoefu kwa siku zijazo. Mkurugenzi Mtendaji ana wajibu wa kuhakikisha kuwa wajumbe wa kamati ya uongozi wana ujuzi, mamlaka na rasilimali za kutosha kutekeleza mkakati wa kampuni.

**Uwajibikaji**

Bodi ina wajibu wa kuhakikisha kampuni inakuwa na mafanikio. Kazi yake ni kuongoza na kutoa maamuzi ya busara katika kuielekeza kampuni kufanikisha ukuaji endelevu na kufanya kazi kwa maslahi ya wanahisa.

**Muundo ufuatao unaonesha safu ya viongozi wa Vodacom Tanzania tarehe 31 Machi 2025**

**Bodi**

**Kamati za Bodi**

- Kamati ya Ujira
- Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji Kamati ya Uteuzi

**Mkurugenzi Mtendaji**

**Mkurugenzi Mtendaji**

- Masuala ya Mahusiano na Taasisi ya Vodacom
- Fedha
- Huduma kwa Wateja
- TEHAMA
- Kitengo cha Biashara: Wateja wa Biashara
- Kitengo cha Biashara – Wateja Binafsi
- Sheria na Udhibiti
- Huduma za Digitali
- Kitengo cha Biashara: M-Pesa
- Dharura na Utekelezaji
- Mtandao
- Rasilimali Watu



Kwa mujibu wa utendaji bora, Mwenyekiti na Mkurugenzi mtendaji wana majukumu tofauti. Mwenyekiti ana wajibu wa kuongoza Bodi, wakati Mkurugenzi Mtendaji anawajibika kusimamia uendeshaji wa kampuni.

**Katiba ya Bodi inaeleza wajibu wa Bodi, ambao ni pamoja na:**

- Kufanya uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji na Mkurugenzi wa Fedha
- Kusimamia kwa karibu mwelekeo wa kimkakati wa kampuni
- Kupitisha miradi mikubwa, ununuzi au mauzo ya vitu
- Kufanya uamuzi wa busara kuhusu masuala ya biashara ya kampuni, mbali na menejimenti
- Kuhakikisha kuwa miundo, sera na taratibu stahiki zinakuwepo
- Kuhakikisha udhibiti wa ndani wa kampuni unakuwa na mafanikio
- Kupitia na kutathmini dharura za kampuni
- Kupitisha bajeti ya mwaka na mpango wa utekelezaji
- Kupitisha matokeo ya pamoja ya fedha ya mwaka na ya muda na vilevile mawasiliano kwenda kwa wadau
- Kupitisha muundo wa uongozi na mpango wa mwendelezo wa uwepo wa viongozi; na
- Usimamizi wa teknolojia ya habari

### Wakurugenzi

Katiba ya kampuni inaeleza kuwa wakurugenzi wanapaswa kustaafu kwa zamu na wanaweza kuchaguliwa tena baada ya kila miaka mitatu.

### Mwenyekiti

Katiba inaitaka Bodi kumchagua Mwenyekiti kila mwaka. Bodi ilimchagua Bwana David Tarimo kuwa Mwenyekiti kuanzia April 1, 2025.

### Kupata ushauri huru

Bodi inatambua kuwa inawezekana kukawa na wakati ambapo wakurugenzi wakaona kuwa ni muhimu kupata ushauri huru wa kitaalamu. Kampuni itagharamia huduma hii kwa mujibu wa utaratibu uliopo.

# Taarifa ya shughuli za uongozi

## Vodacom Tanzania Plc

### Mikutano ya Bodi

Jedwali hapo chini linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi katika mikutano ya Bodi kwa mwaka huu:

| | Mikutano ya Bodi | | (A) Mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | (R) | (N) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jina la Mkurugenzi | Robo mwaka | Maalum | Robo mwaka | Maalum | Mikutano ya Kamati ya Ujira | Mikutano ya Kamati ya Uteuzi | Jumla mahudhurio |
| Jaji (Mstaafu) Thomas B Mihayo (Mwenyekiti) | 4/4 | 3/3 | | | | 5/5 | 12/12 |
| Bi Margaret Ikongo | 4/4 | 3/3 | 4/4 | 3/3 | | | 14/14 |
| Bi Thembeka Semane | 4/4 | 3/3 | 4/4 | 3/3 | | | 14/14 |
| Bi Kanini Mutooni | 4/4 | 3/3 | 4/4 | 3/3 | 4/4 | 5/5 | 23/23 |
| Bi Raisibe Morathi | 4/4 | 3/3 | | | | | 7/7 |
| Bw Nkateko Nyoka | 4/4 | 2/3 | | | | | 6/7 |
| Bw Diego Gutierrez | 3/4 | 2/3 | | | 4/4 | | 9/11 |
| Bw Matimba Mbungela | 4/4 | 3/3 | | | 4/4 | 5/5 | 23/23 |
| Bw Haytham Ammar | 4/4 | 2/2 | | | | | 6/6 |
| Bw Dejan Kastelic | 3/4 | 3/3 | | | | | 6/7 |
| Bw Philip Besiimire | 4/4 | 3/3 | | | | | 7/7 |
| Bi Hilda Bujiku | 4/4 | 3/3 | | | | | 7/7 |
| **Jumla** | **97.9%** | **94.3%** | **100.0%** | **100.0%** | **100.0%** | **100.0%** | **97.8%** |





- Sitholizwe Mdlalose alijiuzulu kuwa mkurugenzi asiye mtendaji kuanzia tarehe 1 Aprili 2024
- Dejan Kastelic aliteuliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji kuanzia tarehe 1 Aprili 2024
- Sudhersan Ramasamy alijiuzulu kuwa mkurugenzi asiye mtendaji kuanzia tarehe 1 Aprili 2024
- Haytham Ammar aliteuliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji kuanzia tarehe 1 Juni 2024

## M-Pesa Limited

### Mikutano ya Bodi ya M-Pesa Limited

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi kwenye mikutano ya Bodi ya M-Pesa Limited mwaka huu:

| | Mikutano ya Bodi | | (A) Mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Jina la Mkurugenzi | Robo mwaka | Maalum | Robo mwaka | Maalum | Jumla Mahudhurio |
| Bw Jaffer Machano (Mwenyekiti) | 1/1 | 1/1 | | | 2/2 |
| Bw Sitoyo Lopokoiyit | 3/4 | 1/1 | | | 4/5 |
| Bw Epimack Mbeteni | 3/4 | 1/1 | | | 4/5 |
| Bw Olaf Mumburi | 4/4 | 1/1 | 4/4 | – | 9/9 |
| Bi Hilda Bujiku | 4/4 | 1/1 | 4/4 | – | 9/9 |
| Bw Philip Besiimire | 4/4 | 1/1 | | | 5/5 |
| **Jumla** | **90.5%** | **100.0%** | **100.0%** | **n/a** | **94.3%** |

* Bw. Machano aliteuliwa kuwa Mkurugenzi huru kuanzia 1 Februari 2025.

### Mgawanyo wa wajumbe wa Bodi ya M-Pesa Limited

**Jinsia**

Wanawake **20.0%**

Wanaume **80.0%**

**Muundo wa Bodi**

Wajumbe 6

1 Mkurugenzi mtendaji

4 Wakurugenzi wasio watendaji

1 Mkurugenzi huru

94.3% Mahudhurio ya vikao vya bodi

**Miaka**

40 – 49: 5

50+: 1

**Muda waliohudumu kwenye nafasi hizi**

Miaka 0-3: 3

Miaka 4-6: 2

Miaka 6+: 1

# Utaratibu wetu wa Ujira

## Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira

Kwa niaba ya Bodi na Kamati ya Ujira, najivunia kuwasilisha ripoti hii ya Ujira ya Vodacom Tanzania kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2025. Ripoti hii inatoa muhtasari wa falsafa yetu ya ujira na jinsi tulivyotekeleza sera yake katika mwaka huu.



Kanini Mutooni

Hapa Vodacom, **ujira unathamini mchango katika thamani tuliyoijenga** ili kuwahamasisha wafanyakazi wetu katika utekelezaji bora wa mkakati wetu na kuishi kwa mujibu wa azma yetu. Sera yetu ya ujira inaweka bayana motisha za muda mfupi na mrefu ambazo tunaamini zitatusaidia kufanikisha azma hii, tukiongozwa na malengo yetu kibiashara. Utaratibu wa motisha za muda mfupi juu ya utendaji, yaliyoidhinishwa mwaka wa fedha 2023, bado yanatumika. Tumeendelea kuzipima taratibu hizo ili kujiridhisha kwamba bado zinatoa motisha sahihi zitakazowezesha kufanikisha malengo yetu ya ukuaji na kuwalinda wateja. Mwaka huu, Vodacom Tanzania imefanya vizuri sana kiutendaji.

Ili kujenga uaminifu na thamani kwa wafanyakazi wetu, pia **tunazingatia manufaa mengineyo mbali na malipo ya kifedha,** ambayo yanatutofautisha na wengine katika soko hili lenye ushindani mkubwa. Ari chanya ya wafanyakazi wa Vodacom Tanzania, na muendelezo wake wa kuongoza katika kundi la makampuni ya Vodafone kwenye kipimo cha Ari ya Timu na Ushirikishwaji wa Wafanyakazi ni kielelezo tosha cha ubora wa mbinu zetu. Juhudi zetu pia, zimetambuliwa nje ya Kampuni kwa kutajwa kuwa mwajiri bora zaidi Tanzania kwa mwaka wa nane mfululizo.

Mwaka huu, Kamati ya Ujira ilitafiti mahitaji ya kisheria Tanzania na vigezo vya kutekeleza mpango wa wafanyakazi wa Vodacom Tanzania kuwa na umiliki wa hisa. Tunaamini jambo hili litaongeza motisha kwa wafanyakazi na uaminifu wao kwa kampuni huku tukihakikisha kuwa wafanyakazi wanaenda sambamba na malengo ya kimkakati ya kampuni. Utekelezaji wa mpango huu kwa msaada wa wanahisa wetu utabaki kuwa eneo muhimu la majadiliano kwa kamati katika mwaka ujao.

Sehemu ya uwajibikaji wetu kama muajiri ni kuhakikisha kuwa **ujira kwa wafanyakazi wetu unazingatia tathmini ya soko.** Mwaka huu, kama sehemu ya mapitio ya kila mwaka ya mishahara, tulichunguza vigezo na mbinu zinazotumika kuamua ujira kwa wafanyakazi wetu. Zoezi hili lilifanyika ili kuhakikisha kuwa vigezo na mbinu zetu ni sahihi na zinaendana na malengo yetu kibiashara na vipaumbele uendelevu. Hili ni muhimu hasa kutokana na ushindani mkubwa wa kiujuzi na kiuongozi katika sekta hii ya mawasiliano ya simu inayobadilika kila leo. Kutokana na tathmini hiyo, Kamati ya Ujira ina imani kuwa Vodacom Tanzania inatoa malipo stahiki ambayo yataendelea kuvutia, kubakiza na kutoa motisha kwa watendaji na wafanyakazi wenye uwezo wa hali ya juu.

Pia, tuliendelea kupiga hatua nzuri katika kuleta **usawa wa kijinsia** mahali pa kazi. Kampuni iliendeleza uwekezaji wake katika kuwawezesha wanawake kupitia programu mbalimbali za uongozi na kuongeza usawa wa kijinsia. Nilivutiwa pia kuona jinsi usawa wa kijinsia ulivyozingatiwa katika mipango ya viongozi wajao wa ngazi za juu. Hili halikuwa zoezi la kujifurahisha tu, bali mjadala makusudi na wa kina wenye lengo la kuona namna wanawake ndani ya shirika wanavyoweza kuendelezwa kuwa viongozi. Juhudi hizi zinaonesha dhamira ya Vodacom Tanzania katika kuhakikisha kuwa kila tunachofanya kinaendana na azma yetu.

Tunapouangalia mwaka ujao, bila shaka kuna changamoto mbalimbali na hali ya sintofahamu ya kisiasa duniani inayoweza kuleta vikwazo visivyotarajiwa kwenye mazingira ya biashara. Hata hivyo, tuna matumaini makubwa na mazingira ya biashara nchini, kutokana na uimara wa uchumi wa ndani unaokua, pamoja na fursa kubwa zilizopo katika eneo la huduma za simu na data.

Tukiwa ni kampuni inayolenga ukuaji zaidi, Vodacom Tanzania imejipanga vizuri kuzifikia fursa za ukuaji, kupitia misingi yake imara ya kuvutia, kukuza na kuhifadhi vipaji ili kuongeza kasi yake katika mwaka ujao.

**Kanini Mutooni**
Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira
15 Julai 2025

Katika kuandaa taarifa hii, kamati imezingatia miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana ('CMSA'), 1994. Tumeridhika kwamba taarifa inaafikiana na miongozo na utawala bora kwa kampuni zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa nchini Tanzania, huku tukiwa waangalifu juu ya taarifa za mtu binafsi au taarifa nyeti za soko.

Tunakuhimiza usome taarifa hii na kutoa maoni yoyote juu ya falsafa na sera ya ujira ya Kampuni.

## Taarifa ya Masuala ya Ujira

Kulingana na miongozo ya Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana kuhusu taratibu za usimamizi wa makampuni ya umma yaliyoorodheshwa nchini Tanzania, taarifa hii inaeleza sera za Vodacom Tanzania za ujira kwa wakurugenzi watendaji na wakurugenzi wasio watendaji hususan kiasi na aina za ujira kwa wakurugenzi ikiwa ni pamoja na wakurugenzi wasio watendaji kwa pamoja.

**Falsafa, sera na mfumo wetu wa ujira kwa mwaka wa fedha 2025 kwa wakurugenzi watendaji:**
Lengo letu ni kuwavutia, kuwawezesha kubaki na kuwapatia motisha watendaji wenye uwezo wa hali ya juu, sambamba na kulinganisha ujira wao na maslahi ya wanahisa na taratibu bora za utekelezaji.

**Utaratibu wetu wa stahiki za ajira ni mpana, wenye ulinganifu kwenye vipengele vifuatavyo:**

- Ujira wa uhakika (GP)
- Motisha ya muda mfupi (STIP)
- Motisha ya muda mrefu (LTIP)
- Programu mbalimbali za utambuzi
- Fursa mbalimbali za kujifunza na kujiendeleza
- Mazingira ya kazi yanayovutia; na
- Programu nzuri ya ustawi wa wafanyakazi

Vipengele hivi vinaendana na kuimarishwa kwa utaratibu wetu wa kutathmini utendaji kazi na kuendeleza vipaji. Sera yetu ni kuwapa marupurupu viongozi wetu watendaji kutokana na michango yao katika ufanisi wetu kimkakati, kifedha na kiutendaji. Ili kuwa muajiri anayeheshimika katika sekta yetu tunahitaji kuvutia, kuendeleza na kubakiza vipaji bora na rasilimali ya wataalamu wa ndani na kimataifa.

Viongozi watendaji wanafuata falsafa ya 'Jumla ya gharama kwa kampuni', ambayo tunairejelea kama ujira uhakika (GP). Michango katika huduma za tiba, fedha za ustaafu na mafao ya bima yamejumuishwa katika GP.

Kila mwaka tunalinganisha viwango na kuongeza malipo katika GP kulingana na soko, ufanisi binafsi na uwezo. Tathmini ya ufanisi binafsi na uwezo wa kiutendaji hubainishwa kupitia utaratibu wetu wa kupima utendaji na uwezo wa kiutendaji wa wafanyakazi wetu. Matokeo ya utaratibu huu, huchangia katika uamuzi wa mabadiliko ya motisha ya muda mfupi na muda mrefu.

Motisha yetu ya muda mfupi inayolipwa kama bonasi ya fedha taslimu hutokana na kufikia malengo kwenye utendaji wa masuala ya fedha, mikakati, uendeshaji wa vitengo na malengo binafsi ambayo kila mtendaji amepewa. Kiasi kilichopo kwa ajili ya motisha ya muda mfupi kinatokana na utendaji kwenye masuala ya fedha kadiri ya malengo yaliyowekwa na kukubaliwa.

Viongozi watendaji ambao wametumwa kufanya kazi Vodacom Tanzania kutoka Vodacom Group Limited, hulipwa motisha ya muda mrefu kwa mujibu wa taratibu za Vodacom Group Limited, ambapo hupewa umiliki wa hisa na mishahara ya hisa. Hii huchochea utendaji unaoakisi umiliki na uaminifu, na huchangia katika lengo la Vodacom la kuwabakiza watendaji hodari. Mfumo huo ni mfumo kamili wa umiliki, na matokeo yake wahusika hupata gawio kutoka siku walipopewa hisa japokuwa thamani ya hisa inaweza tu kupatikana baada ya miaka mitatu na ni kwa kulingana na kiwango ambacho masharti ya kupewa hisa hizo yametimizwa.

### Taarifa za ujira wa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji

#### Ujira wa wakurugenzi watendaji – Malipo ya Uhakika

Ujira wa wakurugenzi watendaji ulifanyiwa mapitio kwa kuzingatia ulinganishi na ujira wa watendaji wengine katika soko, na pia athari za kushindwa kuwabakiza watendaji muhimu katika menejimenti.

Kwa kuzingatia utaratibu/sera ya ujira, taarifa iliyo kwenye toleo hili ni kwa wakurugenzi waliostahili, ambapo maamuzi yote yanayohusu ujira yamefanyika kwa kuzingatia utaratibu wa ujira na kuidhinishwa na wanahisa. Kama ilivyo kwa mwaka uliotangulia, hakuna mabadiliko yaliyofanywa katika utekelezaji wa sera/utaratibu wa ujira katika mwaka wa fedha 2025.

#### Ujira wa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji (kwa dola za Marekani$)

Taarifa za ujira wa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji zimetolewa kwa muhtasari katika jedwali hapo chini na pia zimewasilishwa katika Maelezo 35 katika taarifa za pamoja za fedha na taarifa binafsi za fedha za kampuni (nakala ya kiingereza) yaliyopo katika ukurasa wa 134.

Kiasi hiki ni jumla ya ada kwa dola ya Marekani, ikijumuisha kodi zote pamoja na kodi ya zuio, inayolipwa kwa shilingi ya Kitanzania kwa wakurugenzi wazawa, randi ya Afrika Kusini kwa wakurugenzi wakazi wa Afrika Kusini na dola ya Marekani kwa wakurugenzi wengine. Ada hii inalipwa kila robo mwaka.

| Wakurugenzi | Bodi | Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | Ujira | Uteuzi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| TB Mihayo | 150 000 | | | | **150 000** |
| M Ikongo | 30 000 | 15 000 | | | **45 000** |
| K Mutooni | 30 000 | 8 000 | 12 000 | 3 000 | **53 000** |
| T Semane | 30 000 | 8 000 | | | **38 000** |
| D Gutierrez | 30 000 | | 4 000 | | **34 000** |
| M Mbungela | 30 000 | | 4 000 | 3 000 | **37 000** |
| N Nyoka | 30 000 | | | | **30 000** |
| D Kastelic | 30 000 | | | | **30 000** |
| H Ammar | 30 000 | | | | **30 000** |
| R Morathi | 30 000 | | | | **30 000** |
| H Bujiku | | | | | **–** |
| P Besiimire | | | | | **–** |
| | | | | | **477 000** |



# Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji

**Philip Besiimire**

Vodacom Tanzania ni kampuni inayoongozwa na malengo yaliyojikita katika kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora. Ninafuraha kuripoti kwamba mwaka huu tumepiga hatua kubwa katika kutekeleza lengo hili. Na sasa tukiwa tumekamilisha dira yetu ya 2025, tuko katika nafasi nzuri ya kutekeleza Dira ijayo ya 2030.

## Utendaji wetu wa miaka mitano iliyopita

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, tumetekeleza azma yetu ya kuboresha maisha kupitia teknolojia, na kutimiza malengo yetu ya kibiashara. Mafanikio yetu ni pamoja na:

- Uwekezaji endelevu katika mtandao na mifumo ya TEHAMA wa takriban Shilingi trilioni 2, uliowezesha ongezeko la 14.9% katika idadi ya minara yetu yote, huku minara ya 4G ikiongezeka kwa takribani 150% na watumiaji wa simu janja wakiongezeka kwa zaidi ya 150%.
- Huduma zetu za data yenye kasi zilizokuwa zikiifikia 49.2% ya watu, sasa zinawafikia 69.4% ya watu wote, na kuchangia katika kupunguza ombwe la kidijitali.
- Uwekezaji wetu endelevu katika mtandao umewezesha kukua kwa matumizi ya wateja. Mwaka huu, mtandao wetu ulichakata dakika za mawasiliano ambazo ni 98.7% zaidi ya zile zilizochakatwa mwaka wa fedha 2020, na megabiti za data zilikaribia mara tatu ya zile zilizotumiwa na wateja katika mwaka wa fedha 2020.
- Katika kipindi hiki, idadi ya wateja wetu wote imeongezeka kwa 46%, wateja wa M-Pesa wameongezeka kwa 72.3% na wateja wa data sasa ni 55.8% zaidi ya wale wa miaka mitano iliyopita. Ongezeko hili liliwezeshwa na ongezeko la 13.2% la wafanyakazi wetu.
- Kuanzia hatua ya mwanzo kabisa, sasa tumeunganisha biashara zaidi ya 470 000 kwenye mfumo wetu wa malipo ya kidijitali, tukiiunga mkono ajenda ya serikali ya uchumi usiotumia pesa taslimu na pia kuchochea ukuaji wa uchumi.

Ukuaji wa viashiria hivi vya utendaji uliwezesha ufanisi thabiti wa biashara. Mapato yetu ya huduma yemekua kwa wastani[1] wa asilimia 8.1% kila mwaka huku faida yetu baada ya kodi ikikua kwa ongezeko la wastani wa asilimia 14.6%. Ukuaji huu ni muhimu katika ongezeko la faida kwa wanahisa wetu.

## Tathmini ya mwaka huu

Katika mwaka wa fedha 2025, tuliendelea na dhamira yetu ya **kuiwezesha jamii** kwa kutumia bidhaa na huduma na teknolojia za kibunifu, ili kuleta matokeo chanya kwenye jamii kupitia huduma za mawasiliano na ushirikishaji kifedha.

**Huduma yetu ya M-Pesa ina bidhaa kadhaa wezeshi, zikiwemo:**

- Lipa kwa Simu, inayochochea biashara kwa kuwezesha malipo ya kidijitali
- Mikopo ya kidijitali kama Songesha
- Mikopo ya muda mfupi inayosaidia wateja na wafanyabiashara ndogondogo kutatua changamoto zao za kifedha za muda mfupi

Bidhaa yetu ya uwekezaji, **M-Wekeza,** ilizinduliwa mwezi Novemba 2024 kwa ushirikiano na Sanlam Investments East Africa-Tanzania. Jukwaa hili la uwekezaji kupitia simu ya mkononi linawawezesha wateja kuwekeza na kukuza mali zao kwa urahisi kupitia uwekezaji katika rasilimali za kifedha, unaotekelezwa na wasimamizi wa mfuko. Katika kipindi cha miezi mitano tu tangu kuanzishwa, wateja waliwekeza takriban shilingi bilioni 25, jambo linaloonesha mwitikio mkubwa na imani katika bidhaa hii.

Tulifanikiwa kupiga hatua kubwa katika utumiaji wa huduma yetu ya akiba kwa vikundi, **M-Koba.** M-Koba ina sifa za kipekee za kuhakikisha usalama na uwazi kwa wanachama waliopo katika vikundi vya akiba za kijamii. Suluhisho hili linalomlenga mteja linahamasisha tabia ya kuweka akiba. Katika mwaka wa fedha 2025, akiba za wateja kupitia M-Koba ziliongezeka mara mbili ikilinganishwa na akiba walizoweka mwaka uliopita. Hii ni ishara ya kukubalika kwa huduma hii ya M-Koba kama suluhisho la kuaminika la kulinda akiba za kijamii na kuziwezesha jamii, na hasa wanawake, ambao ndio sehemu kubwa ya wateja wetu wa M-Koba.

Katika azma ya **kuilinda sayari yetu,** tulijikita katika kuboresha miundombinu yetu ili kupunguza matumizi ya nishati na matumizi ya jenereta zinazotumia mafuta, huku tukiongeza matumizi ya nishati mbadala. Tunaendelea kuwekeza katika mifumo inayotumia nishati kidogo katika mtandao wetu, miundombinu ya TEHAMA na ofisi zetu. Juhudi hizi zilichangia katika kupungua matumizi ya nishati kwa megawati 2 861 (ikiwemo megawati 1 500 za matumizi ya umeme), wakati uzalishaji wetu wa hewa ya ukaa (GHG) ulipungua kwa tani 787.6 ($tCO_2e$). Wakati wa ziara ya hisani ya waendesha baiskeli ya Vodacom Twende Butiama ambayo hufanyika kila mwaka, tulipanda miti zaidi ya 50 000. Hii ikiwa ni sehemu ya juhudi zetu za kuchochea utunzaji wa mazingira ili kulinda tabianchi, kupitia jamii inayotuzunguka.

Mahusiano yetu ya uwazi na kiadilifu na wateja na wadau muhimu yanatusaidia kutekeleza malengo yetu katika nguzo ya tatu ya azma yetu inayokusudia **kuendeleza uaminifu.** Falsafa yetu ya uhusiano na wateja imejengwa katika misingi ya uwazi, usalama, kumlinda mteja muaminifu, na ubora wa huduma. Mbali na kazi yetu za kuiwezesha jamii na kuilinda sayari yetu, tulifanya juhudi mbalimbali kudhihirisha dhamira yetu kwa wateja na jamii kwamba sisi ni washirika wao wa kuaminika. Juhudi hizo zilijumuisha kampeni ya namna ya kupunguza matumizi makubwa ya data, vidokezo vya ulinzi wa fedha zilizohifadhiwa kwenye M-Pesa na uhamasishaji kuhusu usalama mtandaoni kwa wanafunzi wa vyuo vikuu.

Mamilioni ya wateja wanatuamini kwa taarifa zao binafsi na rasilimali zao za kifedha kupitia matumizi yao katika mtandao wetu. Hivyo kwetu sisi, kufanya kazi kwa maadili na utii wa sheria ni jambo tunalolipa umuhimu mkubwa. Tunaendelea kuwekeza katika akili mnemba (AI) na mifumo ya kuchanganua tabia ya matumizi ya wateja (CVM) ili kuboresha usalama na faragha katika mtandao wetu. Mwaka huu, tuliendesha programu kwa wafanyakazi wetu, kuwajengea uelewa na kuwasisitiza umuhimu wa usiri na faragha ya taarifa binafsi za wateja. Juhudi hizi zinaenda sambamba na matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Tanzania ya mwaka 2022 (PDPA).

Ninafuraha kwamba Vodacom ilikuwa miongoni mwa taasisi za kwanza kabisa kupata Hati ya Usajili wa Mchakata na Mdhibiti Taarifa, zilizotolewa uzinduzi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi mwezi Aprili 2024, chini ya mgeni rasmi Mheshimiwa Dokta Samia Suluhu Ha ssan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni jambo la kutia moyo kwamba utaratibu wetu za kuendesha biashara kimaadili na kwa kuzingatia malengo unaonekana na kutambuliwa, na kutujengea mahusiano mazuri ya kuaminiana na wadau wetu.

Katika kipindi chote cha mwaka, ufanisi wetu ulipata kutambuliwa na taasisi mbalimbali za udhibiti. Kwa kutaja chache, tulipokea tuzo kutoka Soko la Hisa la Dar es Salaam kwa uendeshaji wetu endelevu wa biashara na nyingine kutoka Bodi ya Taifa ya Waha endelevu sibu na Wakaguzi wa Hesabu – Tanzania, ikitambua ubora wa juu wa taarifa zetu za kifedha.

Mifano hii inaonesha juhudi za timu yetu za kuendelea kuweka malengo yetu kama kiini cha kujitambulisha sisi ni nani, huduma zetu ni zipi, na jinsi tunavyofanya kazi katika soko. Nakukaribisha usome zaidi kuhusu utendaji wetu kuhusina na ahadi zetu zinazoongozwa na malengo ambao umeelezewa katika sehemu mbalimbali za ripoti hii.

**Mwaka huu, tulipiga hatua nzuri ya utekelezaji wa mkakati wetu wa biashara, ambao unalenga kuikuza biashara kupitia fursa za biashara mpya, huku tukiilinda biashara yetu iliyopo.**

Tuliendelea **kukuza huduma ya mawasiliano kwa simu za mkononi,** ambazo bado ni nguzo ya biashara yetu na kichocheo muhimu cha mwendelezo wa kasi yetu ya kibiashara. Tulimaliza mwaka na ongezeko la 15.7% la idadi ya wateja wetu hadi milioni 22.6[1] na ongezeko la 19.0% kwa watumiaji wa data. Kati ya watumiaji wetu wa data, zaidi ya 70% walikuwa watumiaji wa simu janja. Jambo hili lilitupa nafasi pia ya kufanikisha malengo yetu ya kuongeza ushirikishaji wa kidigitali kwa kuwekeza katika mtandao na matumizi ya simu janja. Matokeo yake tulifanikiwa kuimarisha nafasi yetu ya uongozi katika soko tukiwa na 31.9%[2] ya wateja katika soko.

**Mwaka huu, tuliwekeza Shilingi bilioni 175.0 za kitanzania katika** miundombinu, ambazo tulizielekeza katika uboreshaji na upanuzi wa mtandao wetu na kuboresha uwezo wa mifumo yetu ya TEHAMA. Tulijenga minara mipya 471 ya teknolojia ya 4G, ikiwemo minara 126 tuliyo shirikiana na mfuko wa mawasiliano kwa wote – Universal Communications Service Access Fund (UCSAF), ili kupeleka mawasiliano katika maeneo ambayo hayajahudumiwa vya kutosha. Tulikamilisha maboresho ya kuongeza uwezo kwenye minara 286 ya teknolojia ya 4G ili wateja wetu waendelee kufurahia huduma zetu za data katika ubora wa hali ya juu. Pia, tuliweka juhudi zilizopelekea ongezeko la 33.4% la idadi ya watumiaji wa simu janja kwenye mtandao wetu . Matokeo haya yalichagizwa na ushirikiano na washirika wetu kibiashara na pia huduma yetu ya kukopesha vifaa vya mawasiliano. Uwekezaji wetu endelevu, pamoja na ongezeko katika matumizi ya simu janja, vilisaidia kuwa na ongezeko la karibu 50% la matumizi ya data kwa teknolojia ya 4G, huku mtandao wetu wa 4G ukibeba zaidi ya 80% ya megabiti zote za data zilizotumika katika mtandao wetu. Mabadiliko haya ya matumizi ya data kwenda teknolojia za kisasa zaidi ni muhimu katika kupunguza msongamano katika miundombinu ya teknolojia za chini na kuimarisha ubora wa huduma kwa wateja wetu.

Tuliendelea kutoa mchango mkubwa katika kupunguza ombwe la kidijitali nchini, na kuhamasisha ushirikishaji wa kifedha kwa **kupanua na kuongeza kasi ya ukuaji wa M-Pesa.** Kama ilivyoelezwa awali, M-Pesa ni huduma muhimu kwetu katika utekelezaji wa azma yetu na pia ni kichocheo kikuu cha ukuaji wa mapato yetu ya huduma na kuleta vyanzo mbadala vya mapato. Mafanikio haya yamechagizwa na matokeo mazuri katika viashiria vyote vya msingi,vikichochewa na ushirikiano na washirika wetu. Mapato ya M-Pesa yaliongezeka kwa 29.3%, yakichochewa na ongezeko la 33.8% katika thamani ya miamala iliyochakatwa pamoja na ongezeko la wateja.

Pamoja na ukuaji wa huduma zetu kuu za kutuma na kupokea pesa na miamala ya kuweka na kutoa pesa, tulielekeza juhudi katika kukuza huduma zetu mpya, na ninafurahishwa na matokeo yaliyopatikana.

- Idadi ya watumiaji wa huduma za kifedha za kisasa katika M-Pesa, ikijumuisha mikopo, akiba na bima, ilikua kwa 14.8%
- Mfumo wetu wa malipo wa Lipa kwa Simu ulifikisha zaidi ya biashara 470 000, na ulichakata wastani wa malipo ya zaidi ya shilingi trilioni moja kwa mwezi, ikiwa ni ongezeko la zaidi ya 50%
- Makusanyo ya serikali kupitia zaidi ya akaunti 800 za ukusanyaji mapato zilizopo katika M-Pesa yaliongezeka kwa karibu 30%
- Karibu shilingi trilioni tatu zilikopeshwa kwa takriban nusu ya wateja wetu wa M-Pesa na wafanyabiashara kadhaa kupitia Songesha na mikopo ya muda mfupi, ambapo zaidi ya nusu ya mikopo hiyo ilizinufaisha biashara ndogo ndogo na kuziwezesha kuendeleza shughuli zao za kila siku.

Ukuaji wa huduma za M-Pesa unaakisi kukubalika kwake kama kichocheo cha uchumi salama usiotumia pesa taslimu katika malipo, na uthabiti wake kama zana ya uwezeshaji kiuchumi, hasa kwa watu wasio na akaunti za benki.

Tumeendelea na juhudi zetu za kupanua **huduma za data majumbani na maofisini**, pamoja na **ubunifu na uongozi katika huduma zetu kwa wateja wa kibiashara** – eneo ambalo bado ninaliona lina fursa nyingi za ukuaji.

1 Imekokotolewa kwa kutumia kiwango cha wastani wa ukuaji kwa mwaka (annual compounded interest) wa kipindi cha miaka mitano.

1 Kadri ya tafsiri ya neno "wateja" kwa mujibu wa kanuni ya Kundi la makampuni ya Vodacom.
2 Kwa mujibu wa takwimu za mawasiliano za robo mwaka za Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania za Machi 31, 2025.




## Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji inaendelea

**Huduma zetu kwa wateja wa kibiashara** zilifanya vizuri sana mwaka huu, zikichagizwa na upanuzi wa huduma za data majumbani na maofisini. Kupitia uwekezaji wetu endelevu, unaotoa suluhisho la uunganishaji wa huduma za data kwa maofisi na majumbani nchini kote, tulifanikiwa kuongeza idadi ya wateja wetu wa huduma hii kwa zaidi ya 40%. Kwa namna ya kipekee, uwekezaji wetu unaolenga kukidhi mahitaji ya biashara ndogo na za kati umeonesha mafanikio ya kutia moyo. Tumeendelea kuona uwezekano wa kukuza mfumo wetu wa vitu vilivyounganishwa kwa intaneti (IoT), ambao unatoa fursa za kutoa huduma zinazohusiana na ufuatiliaji katika sekta mbalimbali, ikiwa ni pamoja na huduma za umma, usafiri, biashara na kilimo.

Kwa upande mwingine, tunaendelea kupiga hatua nzuri katika **biashara ya ukodishaji wa sehemu ya rasilimali** katika mtandao wetu, mkongo wa mawasiliano, uhifadhi taarifa kielektroniki na vituo vya data. Eneo hili linaonesha uwezekano mzuri wa fursa za ukuaji. Katika mwaka huu, tumeendelea kuongeza idadi ya wateja, hasa katika huduma za kuwaunganisha watoa huduma za intaneti (ISPs) nchini Tanzania.

Utekelezaji wetu mzuri kibiashara kulingana na vipaumbele vyetu vya kimkakati ulituwezesha kuendelea na nafasi yetu ya uongozi katika kipimo cha kuridhika kwa wateja (NPS) kwa mwaka mzima. Tulimaliza mwaka tukiwa na uongozi thabiti wa makumi ya alama za asilimia, juu ya mshindani wetu wa karibu. Matokeo haya yanaonesha uwezo wetu wa kuendeleza na kutumia **nafasi ya chapa yetu,** huku tukiongeza kuaminika kwa chapa yetu miongoni mwa wadau wetu kwa kuendelea kuboresha zaidi huduma kwa wateja, kuijenga miundombinu yetu ya mtandao kwa mahitaji ya siku zijazo na kutimiza azma yetu.

> Utekelezaji wa kuridhisha wa mkakati wetu ulisababisha matokeo mazuri kifedha.

Mapato ya huduma yaliongezeka kwa 20.5%, yakichagizwa na ongezeko la wateja na ongezeko la matumizi ya huduma zetu. Kinachotia moyo zaidi ni ongezeko kubwa la mapato katika nguzo zetu kuu za ukuaji za M-Pesa, ambayo yalikua kwa 29.3%, na huduma za data za simu ambazo ziliongezeka kwa 21.6%. M-Pesa pia inaongeza wigo wa vyanzo vya mapato yetu kutokana na kiwango kikubwa cha ukuaji wa mapato kutoka huduma zake mpya ikilinganishwa na ukuaji wa huduma asilia. Ukuaji huu unaweka msingi mzuri kwa ukuaji endelevu wa mapato ya huduma. Hatua zetu za kudhibiti matumizi zilisaidia kuokoa gharama za zaidi ya Shilingi bilioni 59.2. Upunguzaji huu wa matumizi pamoja na ukuaji wa mapato yetu,vilichochea ongezeko la faida ya uendeshaji kwa 55.0% na ongezeko la faida baada ya kodi kwa 69.4% hadi kufikia Shilingi bilioni 90.5.

Kwa kuzingatia utendaji huu mzuri wa kifedha, tunapata nafasi kuishauri Bodi ipendekeze **gawio sawa na 50% ya faida yetu baada ya kodi**, kulingana na sera yetu ya gawio.

### Matarajio yetu ya baadae

**Tunatarajia** muendelezo wa mazingira mazuri ya kisiasa na udhibiti wa sekta ambayo yataendelea kuweka mazingira rafiki kwa uwekezaji na shughuli za kibiashara, na kutupatia fursa ya kuendelea kuwaunganisha Watanzania wengi zaidi kwa kesho iliyo bora kadri ya dira yetu ya 2030.

Dira yetu ya 2030 imejikita katika azma yetu ya kuiwezesha jamii, kulinda sayari na kuendeleza uaminifu. Tunakusudia kuendelea kuboresha huduma kwa wateja, kuleta huduma bunifu kwa ajili ya ukuaji na kuweka katika vichocheo vya kimkakati vya kuwezesha ukuaji na ufanisi. Kwa mtazamo huu na mazingira rafiki, tutakuwa katika nafasi nzuri ya kuendelea kukua katika huduma zetu za mawasiliano kwa simu, M-Pesa na huduma kwa wateja wa kibiashara. Nina matumaini makubwa kuhusu fursa zilizopo za kuikuza zaidi biashara yetu ya ukodishaji wa sehemu ya rasilimali zetu,mifumo yetu ya vitu vilivyounganishwa kwenye intaneti (IoT) na huduma za data maofisini na majumbani.

Tunakusudia kuboresha wigo wa huduma zetu kwa ushirikiano na wabia wetu kibiashara ili kuwezesha Watanzania wengi zaidi kufikiwa na huduma za mawasiliano na za kifedha kupitia M-Pesa. Hii inaendana vyema na Mkakati wa Serikali wa Uchumi wa Kidijitali wa mwaka 2023-2033. Pia tunawekeza katika mifumo ya akili mnemba na mifumo ya kuchanganua tabia ya matumizi ya wateja (CVM) ili kuwapatia wateja wetu huduma zinazoendana na mahitaji yao huku tukihakikisha usiri na faragha ya taarifa zao binafsi.

Kuwa na mtandao wa data wa kuaminika ni jambo muhimu katika kuongeza upatikanaji wa huduma za kidijitali. Tutaendelea kujenga na kutumia ushirikiano uliopo ili kutekeleza na kuwaunganisha Watanzania wengi zaidi na dunia ya kidijitali. Katika kuharakisha hili, tutaendelea kuhakikisha kuwa wateja wanapata simu janja kwa bei nafuu kupitia njia za moja kwa moja na ushirikiano na washirika wetu.

Tumejizatiti katika shughuli za biashara endelevu, tukisaidia sekta kuwa thabiti na yenye ushindani wa haki. Tutaendelea kudhibiti gharama zetu za uendeshaji ili kuongeza faida, huku tukiwawezesha wanawake kupitia fursa sawa Pia tutaendelea kuchangia katika kulinda mazingira.

### Shukrani

Tunapofurahia matokeo mazuri, ni muhimu kutambua mchango wa wale waliotuongoza. Kwanza kabisa, Mwenyekiti wetu wa Bodi anayeondoka, Jaji mstaafu Thomas Mihayo ambaye ameonesha uongozi na utumishi bora kwa kampuni. Na sasa baada ya miaka mitano kama Mwenyekiti, Jaji Mihayo ameamua kujiuzulu kutoka katika nafasi hiyo na kustaafu. Kwa niaba ya familia ya Vodacom, ninatoa shukrani zetu kwa kujitolea kwake na kazi yake kubwa kwa miaka yote. Ameacha nyuma biashara imara, inayoongozwa na malengo, na yenye kasi nzuri ya maendeleo. Wakati huo huo, tunamkaribisha kwa moyo mkunjufu Mwenyekiti wetu mpya wa Bodi, Bwana David Tarimo.

Ninapenda pia kutoa shukrani zetu za dhati kwa Bwana Sudhersan Ramasamy na Bwana Diego Gutierrez kwa utumishi wao katika Bodi. Bwana Ramasamy alijiuzulu mnamo Aprili 2024 kama sehemu ya mabadiliko ya kawaida katika uongozi, kulingana na majukumu yake katika Kampuni yetu mama ya Vodacom, wakati Bwana Gutierrez alijiuzulu mnamo Mei 2025 kuendelea na shughuli nyingine nje ya familia ya Vodacom. Tunafurahi kumkaribisha Bwana Haytham Ammar katika Bodi, akichukua nafasi ya Bwana Sudhersan, na tunatarajia kupata mchango wake mkubwa katika kuendeleza kampuni yetu.

Mwisho, ninamshukuru kila mtu katika kampuni na washirika wetu waliochangia katika kufanikisha mafanikio yetu. Kwa pamoja, tutaendelea kuwapatia wateja wetu huduma bora zaidi, huku tukizalisha faida inayoongezeka kwa wanahisa wetu.

Ninatarajia safari nyingine yenye mafanikio katika mwaka ujao, ambao ndio mwaka wa mwanzo katika miaka mitano ya Dira yetu 2030. Tuna mkakati sahihi, uwezo stahiki na timu madhubuti ya kuendeleza kasi yetu na kusaidia azma yetu ya kuwaunganisha Watanzania kwa kesho iliyo bora kupitia biashara yetu msingi ya mawasiliano na huduma za kifedha kupitia M-Pesa.

Tuendelee kujituma kwa moyo wote – pamoja tunaweza!

**Philip Besiimire**
Mkurugenzi Mtendaji
15 Julai 2025



# Utendaji unaozingatia azma yetu

Azma ya Vodacom – ya kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora –maana yake ni kutumia bidhaa na huduma zetu kuwawezesha watu na biashara kustawi. Ili kutekeleza azma hii, masuala ya mazingira, jamii na utawala ni lazima tuyafanye kuwa sehemu ya uendeshaji wetu wa kila siku wa biashara.

Hapa Vodacom, masuala ya mazingira, jamii na utawala (ESG) si mkakati tofauti au shughuli nyingine za ziada, bali ni sehemu ya shughuli za utekelezaji wa mkakati na uendeshaji wa kila siku wa kampuni.

Muongozo wetu wa masuala ya ESG, unaelekeza jinsi ya kukabiliana na mambo yanayohusu ESG kwa kuzingatia fursa, miongozo na utaratibu, ili kuendana na mabadiliko ya kanuni, viwango na matarajio ya wadau wetu kuhusu masuala haya.

Kwa kuzingatia vipaumbele vya kuiwezesha jamii, kulinda mazingira na kuendeleza uaminifu, tumeweka malengo ya ESG yanayo enda sambamba na matarajio ya kitaifa na kimataifa, tukionyesha thamani halisi na kujenga uaminifu kwa wadau.




**Kupitia shughuli zetu katika maeneo haya, tunatoa mchango chanya kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) yafuatayo:**




Malengo ya Maendeleo Endelevu yanatoa maelezo yaliyokubaliwa kimataifa kuhusu jinsi mustakabali wa maendeleo bora unavyopaswa kuwa, yakibainisha ajenda ya muda mrefu ya kutokomeza umaskini, kulinda sayari yetu na kuhakikisha ustawi kwa wote ifikapo mwaka 2030. Kama kampuni tanzu ya kampuni ya mawasiliano inayoongoza barani Afrika, Vodacom Tanzania imejizatiti kutumia teknolojia na rasilimali zake kufikia malengo haya na kusaidia serikali, jamii, biashara na watu binafsi kujenga mustakabali bora. Pia tunachangia katika Dira ya Tanzania 2025 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano kupitia shughuli zetu katika maeneo haya.



Thamani iliyojengwa | Thamani iliyopungua | Thamani endelevu

**Taarifa ya utendaji wetu kwa kila nguzo ya azma yetu tumeitoa kwa ufupi katika kurasa zinazofuata za taarifa hii.**

Unaweza kupata taarifa zaidi katika muhtasari wetu wa masuala ya mazingira, jamii na utawala (ESG) kwenye tovuti yetu.

## Kuiwezesha jamii

Vodacom ina lengo la kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma. Tunaamini katika nguvu ya matumizi ya huduma za mawasiliano na huduma za kidijitali katika kujenga ustahimilivu wa kiuchumi.

Ombwe la kidijitali linabaki kuwa kikwazo kikubwa kwa maendeleo, huku kukiwa na utofauti wa upatikanaji wa elimu, ajira na mawasiliano. Jamii nyingi zinakosa zana, mifumo, na mipango inayohitajika ili kushiriki ipasavyo katika uchumi wa kidijitali, huku kukiwa na upatikanaji mdogo wa huduma muhimu kama vile huduma za afya, elimu na mawasiliano ya kisasa, na hivyo kuathiri ubora wa maisha kwa ujumla.

Barani Afrika, ushirikishaji wa kidijitali unakwamishwa na upungufu wa upatikanaji wa uhakika wa miundombinu ya kidijitali katika maeneo ya vijijini na maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma za mawasiliano, pamoja na gharama kubwa za vifaa na huduma. Teknolojia ya simu za mkononi inavunja vikwazo hivi kwa kuwapa mabilioni ya watu njia yao kuu ya mawasiliano, kupata intaneti na huduma nyingi za kuboresha maisha ikiwa ni pamoja na huduma za elimu, afya na fedha.

### Utendaji wetu kwa Mwaka wa Fedha 2025

#### Kupunguza ombwe la kidigitali

Tunawekeza katika miundombinu ya mtandao ili kutoa huduma ya mawasiliano yenye ubora kwa watu na jamii. Tunaongeza wigo wa mtandao wetu maeneo ya vijijini na kuisaidia jamii kuutumia kwa kuwezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano, vifaa na mifumo kwa gharama nafuu.

- ☑ Tulindelea kuongeza kasi ya kujenga minara ya 3G, 4G na 5G, iliyopelekea huduma zetu za mtandao wa data wenye kasi kuifikia 69.4%[1] ya Watanzania.
- ⊜ Tumeendelea kukuza ushirikishaji kidijitali kupitia vifurushi vyetu vya bei nafuu vya "Ya Kwako tu". Zaidi ya wateja milioni 10.2 walitumia vifurushi hivi vya bei nafuu katika mwaka huu.
- ⊜ Tumeendelea kuwezesha upatikanaji wa simu janja kupitia ushirikiano na wauzaji, na pia kupitia huduma ya simu za mikopo zenye utaratibu rahisi wa malipo. Hatua hizi kwa Pamoja zimewawezesha wateja wetu na kuchochea ongezeko la 33.4% la watumiaji wa Simu Janja kwenye mtandao wetu.

#### Ushirikishaji kifedha

Tunatoa huduma za M-Pesa ambazo zinawawezesha wateja wetu kupata huduma za kifedha bila kuhitaji kuwa na akaunti ya benki. Wateja wengi hawana akaunti za benki na bila M-Pesa, wangeshindwa kupata huduma hizi muhimu.

- ☑ Tuliendelea kuwezesha ushirikishaji wa kifedha kupitia wateja wa M-Pesa, tukiwa na ongezeko la 13.3% la wateja katika mwaka huu.
- ☑ Tulizindua M-Wekeza, huduma ya kipekee ya uwekezaji kupitia simu ya mkononi, na pia tuliiunganisha aplikesheni ya soko la hisa la Dar es salaam (DSE), na kuiwezesha kupatikana moja kwa moja katika super-app ya M-Pesa. Huduma zote mbili zimeleta mageuzi ya upatikanaji wa fursa za uwekezaji kwa Watanzania.



1 Imepimwa katika cha Mbps 3.




## Kusaidia jamii

Tunauza bidhaa na huduma zinazotatua changamoto mbalimbali za kijamii kama vile upatikanaji wa elimu, usawa wa kijinsia, ushirikishwaji kifedha na kuondoa umasikini.

- Mwaka huu, Vodacom Tanzania Foundation ilishirikiana na Taasisi ya Asasi za Kiraia kama mdhamini mkuu wa wiki ya Asasi za Kiraia (AZAKI). Tuliratibu midahalo na majadiliano mbalimbali na asasi za kiraia, tukijikita kwenye nguzo kuu za muongozo wetu wa masuala ya mazingira, jamii na utawala unaoongozwa na azma yetu, ili kutafakari jinsi tunavyoweza kuongeza ushirikiano na kujenga pamoja masuluhisho sahihi kwa Watanzania. Kwa kutambua uwezo wa vijana na nafasi yao kama viongozi wa baadaye na waleta mabadiliko, tuliwaalika Mawakili vijana zaidi ya 1 800 kuhudhuria kwenye wiki ya Asasi za Kiraia. Vijana hawa walipata fursa ya kukutana na kushiriki katika vikao na kushirikiana na asasi za kiraia. Vodacom Tanzania Foundation ilidhamini waleta mabadiliko 30 ambao walipatiwa mafunzo kutoka asasi waliyoichagua, ambapo vijana watatu walichaguliwa kuendeleza suluhisho bunifu la kiteknolojia ili kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya Tanzania.
- Kwa kushirikiana na kampuni ya Huawei, mwezi Oktoba 2024 tulizindua gari-darasa (DigiTruck). Huu ni mradi wa darasa linalotembea kwa lengo la kutoa elimu ya fedha na mafunzo ya ujuzi wa kidijitali hapa Tanzania, hasa kwa wanawake na vijana katika maeneo nje ya miji. Tathmini tuliyoifanya kabla na baada ya utekelezaji wa mradi huu katika mikoa mbalimbali ilituwezesha kuhakikisha kwamba kozi na vifaa tunavyotoa vinakidhi mahitaji ya wanufaika hawa. Pia tulizindua mfumo wa kujifunzia mtandaoni ili kuunganisha nguvu na matumizi ya gari darasa. Mradi huu utaendeshwa kwa miaka mitatu, na tunatarajia kuifikia mikoa 10 kwa mwaka. Tangu kuzinduliwa kwake, mradi huu umewafikia wanufaika 4 387 katika mikoa 12, dhidi ya lengo la wanufaika 5 000 kwa mwaka.
- Jukwaa la elimu la kidigitali la e-Fahamu lilisitishwa kutokana na muitikio mdogo na changamoto za kukuza matumizi yake. Tunafanya tathmini ya namna ya kuanzisha utaratibu mwingine unaofanana na huo kwa siku za baadaye, lakini utakaokua na ufanisi zaidi.
- Kwa kushirikiana na Kampuni za Huawei na MassChallenge, tulikamilisha kwa mafanikio makubwa msimu wa tatu wa mpango wetu wa "Digital Accelerator" wa miezi mitatu, tukishirikiana na kampuni changa 20, na kutumia Shilingi 0.7 bilioni katika mpango huu. Washiriki saba katika fainali walipatiwa semina, vipindi vya ushauri na ziara ya mafunzo huko Shenzhen, China kwa lengo la kuchochea mawazo mapya na fursa kwa Tanzania.
- Matukio mengine katika mwaka wa fedha 2025 ni pamoka na kuanzishwa mpango wa "TechStart" unaolenga kuwaongezea ujuzi vijana milioni 1 wa kiafrika ifikapo mwaka 2027 uliozinduliwa na kampuni yetu mama ya Vodacom Group – Afrika Kusini, Pia tulizindua Jukwaa la Vijana "VYB" linalowapa fursa vijana wa Kitanzania na mpango wa udhamini wa masomo kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati.

**Mfano halisi**

### Matokeo chanya ya wafanyakazi wetu kujitolea: kutoka mahali pa kazi hadi kwenye jamii

Hapa Vodacom Tanzania, mpango wa wafanyakazi wetu kujitolea unaakisi azma yetu na ahadi yetu ya uwajibikaji kwa jamii. Mpango huu unawawezesha wafanyakazi kuchangia katika jamii kwa njia ya kutoa sehemu ya mshahara wao, kuchangisha fedha au kujitolea, ikiwa ni pamoja na kushiriki katika shughuli ambazo wanaweza kutumia ujuzi na utaalamu wao ili kuleta matokeo chanya na ya wazi katika maisha ya watu wengine.

Mwaka huu,
wafanyakazi wetu walifanya shughuli za kujitolea kwa jumla ya masaa
**43 683** kupitia
matukio mbalimbali ikiwa ni pamoja na mbio za hisani za baiskeli za Twende Butiama na kambi zetu za matibabu za jamii.




Ushiriki wa wafanyakazi katika mpango wetu wa kujitolea umeongezeka kwa kiasi kikubwa katika mwaka wa fedha 2025, na tunatazamia ushirikiano na wadau mbalimbali ili kuwafikia watu wengi zaidi mwaka ujao.





Thamani iliyojengwa | Thamani iliyopungua | Thamani endelevu

## Kuilinda sayari

Tunalenga kupunguza athari za shughuli zetu za moja kwa moja kwa tabianchi na mazingira, pamoja na shughuli za washirika wetu, tukiwahamasisha wengine kupunguza uzalishaji wao wa hewa ya ukaa, kuboresha ufanisi wa matumizi ya rasilimali na kulinda mazingira.

Ikiwa ni bara lenye uhimilivu mdogo zaidi wa mabadiliko ya tabianchi, Afrika inaathiriwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya tabianchi. Pamoja na athari za kiuchumi, kijamii na kiafya, mabadiliko ya tabianchi yamesababisha matatizo ya kiekolojia. Ingawa hatua za kiserikali zinahitajika, makampuni ya kibiashara pia yanapaswa kushirikiana na sekta ya umma, kupunguza utoaji wa hewa ya ukaa na kuchangia kutafuta suluhisho juu ya changamoto za mabadiliko ya tabianchi na mazingira.

Nguzo yetu ya kuilinda sayari inaakisi matamanio yetu ya kuwa kinara katika uendeshaji biashara endelevu. Mkakati huu unajumuisha msimamo wetu wa kuwa na uzalishaji mdogo wa hewa ya ukaa siku zijazo na unazingatia asili na bioanuwai katika shughuli zetu moja kwa moja na katika shughuli za washirika wetu katika mnyororo wa thamani. Tunawasaidia wateja wetu, wasambazaji na wadau wengine kujenga tabia ya kutumia mbinu zinazolinda sayari yetu. Tunaunga mkono jambo hili na kuongoza kwa mfano, tukibadilisha mbinu zetu kuwa endelevu zaidi, kwa mfano, kwa kutumia teknolojia za kidijitali ambazo ni rafiki kwa mazingira.

Tunaamini pia kwamba jamii inahitaji kuelekea uchumi wenye ufanisi zaidi na wa mzunguko unaolenga kupunguza takataka. Mkakati wetu wa usimamizi wa taka na matumizi endelevu, unalenga kupunguza madhara ya taka zitokanazo na vifaa vyetu vya mtandao pamoja na vifaa vya kielektroniki tunavyoviuza na vinavyotumiwa na wateja wetu.

### Utendaji wetu wa mwaka wa fedha 2025


#### Kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi

Mabadiliko ya tabianchi yanahatarisha shughuli zetu na za washirika wetu katika mnyororo wa thamani. Tunakabiliana na janga hili la kimataifa kupitia juhudi zetu za kupunguza na kushughulikia athari na hatari zinazohusiana na tabianchi.

- Mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira yanaongeza hatari kwa Tanzania kukumbwa na mafuriko, ukame, matetemeko ya ardhi, maporomoko ya ardhi na hali ya mawimbi makubwa baharini. Katika hili, Vodacom Tanzania inashirikiana na serikali na Shirika la Msalaba Mwekundu Tanzania kufanya utafiti wa watumiaji ili kuandaa mkakati wa kitaifa wa mfumo wa tahadhari za mapema kwa njia ya simu (EWS)[1]. Mfumo huu wa kutoa tahadhari utasaidia jamii kujiandaa na kukabiliana na matukio ya hali mbaya ya hewa na madhara kwa mazingira. Wakati wa awamu ya kwanza, tulifanya utafiti huko wilayani Kilosa na kushirikiana na jamii ya pale ili kufahamu mahitaji na uchaguzi wa njia bora na namna ya kutoa taarifa za Mfumo wa Kutoa Tahadhari za hali ya hewa.

#### Kutekeleza operesheni za kupunguza kiwango 1 na 2 cha uzalishaji wa hewa ya ukaa

Tunapoelekea katika jamii ya kidijitali zaidi, huku matumizi ya intaneti na data za simu yakiongezeka, kadri ya malengo ya kundi la ampuni yetu mama ya Vodacom Group ya Afrika Kusini, tumejizatiti kufanya bidii kuelekea kukomesha uzalishaji wa hewa ya ukaa kufikia sifuri katika shughuli zetu, na kushirikiana na wadau wengine katika sekta ya umma na binafsi kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa katika sekta ya mawasiliano barani Afrika.



1 Ili kuchochea uwezo wa mawasiliano ya simu kuokoa maisha kupitia mifumo ya tahadhari za mapema (EWS), GSMA ilitoa ahadi ya sekta ya mawasiliano katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2023, COP28. Vodafone ni mmoja wa waliotia saini ahadi hiyo ya sekta, ambayo inalenga kutimiza azma ya kufanikisha upatikanaji wa EWS kwa wote kupitia Mpango wa EW4All.



- Mwaka huu tuliunganisha minara 74 kwenye gridi ya taifa ambayo hapo awali ilikuwa inatumia majenereta za dizeli kupata umeme. Lengo ni kupunguza matumizi ya dizeli na athari zake kwa mazingira. Tunaendelea kuchukua hatua za kupunguza matumizi ya majenereta ya dizeli kadri inavyowezekana katika kuendesha minara yetu. Changamoto bado zinakuwepo katika maeneo ya mbali ambapo umeme wa gridi haupatikani.
- Tuliendelea kutekeleza miradi inayolenga kupunguza athari zetu kwa mazingira na uzalishaji wa hewa ya ukaa. Mwaka huu, tumefanikiwa kupunguza matumizi yetu ya umeme kwa megawati 1 500 (megawati 2 861 tukijumuisha na nishati kutoka matumizi ya dizeli), na kupunguza uzalishaji wetu wa hewa ya ukaa kwa tani 787.6 ($tCO_2e$). Mafanikio haya yalipatikana kupitia:
  - Uboreshaji wa mifumo ya kupooza joto katika vituo vya Data vya Kwale na Dodoma
  - Kuweka taa mpya za LED zenye vihisio vya uwepo katika vituo vyote vya Data
  - Kuondoa vifaa visivyotumika au ambavyo vimefikia mwisho wa matumizi yake katika vituo vitatu vya Data
  - Kuunganisha umeme wa gridi katika minara ambayo hapo awali ilikuwa ikitumia majenereta ya dizeli

## Kuchochea matumizi endelevu

Taka za kielektroniki ni miongoni mwa vyanzo vya uchafuzi wa mazingira vinavyoongezeka kwa kasi zaidi duniani. Hivyo, kuhamasisha matumizi endelevu ya vifaa vya kielektroniki ni muhimu katika kulinda mazingira. Matumizi endelevu yanazingatia mzunguko mzima wa maisha wa rasilimali hiyo unalenga kuondoa taka – hivyo kupunguza athari za mazingira.

- Kama kampuni inayowajibika kwa jamii, Vodacom Tanzania inatimiza matakwa ya sheria ya tozo ya mazingira iliyowekwa kwenye vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki vinavyoingizwa Tanzania ili kuhakikisha uteketezwaji sahihi wa vifaa hivyo vinapofikia mwisho wa matumizi. Tozo hii inalenga kuwezesha uteketezaji na urejeshaji sahihi wa taka za kielektroniki, sambamba na kanuni ya uwajibikaji wa mtengenezaji hadi kufikia mwisho wa mzunguko wa uhai wa bidhaa.
- Mipango yetu ya kutumia rasilimali kwa ufanisi na usimamizi wa uteketezaji taka inapunguza athari kwa mazingira zinazotokana na mtandao wetu na taka za kielektroniki. Taka za kielektroniki huondolewa kwenye maghala kupitia mchakato wa mnada, ambapo wateketezaji taka walioidhinishwa hununua taka hizo na kuzichakata ili kuweza kupata vifaa ambavyo vinaweza kutumika tena na kisha husimamia uteketezaji wa mwisho wa taka hizo kwa njia sahihi, kulingana na taratibu na miongozo ya kimazingira. Hii inachangia katika utunzaji wa mazingira, na kusaidia katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

## Utunzaji wa bioanuwai

Dunia inakabiliwa na kuporomoka kwa kasi kwa mazingira asilia, huku takribani spishi milioni moja zikiwa hatarini kutoweka. Ijapokuwa athari zetu za moja kwa moja kwenye bioanuwai ni ndogo, tunalenga kuelewa kiwango chake na kupunguza athari za kimazingira za muonekano wa miundombinu yetu. Tunaweza pia kutumia teknolojia ya kidijitali kuwezesha hatua na mipango ya kulinda, kusimamia na kurejesha mazingira asilia.

- Mwaka huu, tulishiriki kuandaa Mbio za baiskeli za hisani za mwaka 2024 za Twende Butiama, ambapo waendesha baiskeli walishiriki katika kampeni ya kutoa elimu juu ya mabadiliko ya tabianchi.
- Kampeni zetu za uhamasishaji wa Siku ya Mazingira Duniani zilitumia majukwaa ya mitandao ya kijamii kuhamasisha uelewa wa mazingira na uendelevu.
- Zaidi ya hayo, mwaka huu, tulichangia miti 20 000 kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika juhudi zake za kukuza bioanuwai kupitia mpango wake wa Tanzania ya Kijani.

## Kuendeleza uaminifu

Utii wa sheria, maadili na uadilifu ni muhimu kwa mafanikio yetu ya muda mrefu, na ndio msingi wa uendeshaji wa biashara yetu. Uwazi, uaminifu na uwajibikaji ni mambo yanayotuongoza katika mahusiano yetu kibiashara. Tunaendelea kukuza nguvukazi anuwai na jumuishi ya kimataifa ambayo inaakisi wateja na jamii tunazohudumia.

Kwa wateja wetu, tunalinda taarifa zao, kuhakikisha kuwa huduma zinatolewa kwa usalama na kwa uwajibikaji, na kutoa mwongozo kuhusu namna ya kutumia teknolojia mpya kiuadilifu. Tunakuza utamaduni thabiti wa kulinda afya na usalama, na tunakusudia kuheshimu haki za binadamu katika shughuli zetu na kusimamia kwa makini athari na hatari mnyororo wetu wa thamani. Katika kulinda viwango vya juu vya sekta, tunafanya kazi kwa kuwajibika na kwa uwazi, tunatii viwango vya kisheria na kanuni, na kuhakikisha kwamba wafanyakazi, washirika wa biashara na wasambazaji wanatenda kazi kwa usahihi.

### Utendaji wetu katika mwaka wa fedha wa 2025

## Uadilifu katika biashara

Kudumisha na kuimarisha uaminifu ndio msingi wa azma yetu. Tunawawajibisha wafanyakazi wetu, washirika wa kimkakati na kibiashara pamoja na wasambazaji kwa kuhakikisha wanafanya kazi kwa viwango vya juu vya uadilifu.

- Tumeanzisha uhusiano wa karibu na ofisi za mikoa na wilaya, ikiwa ni pamoja na kuanzisha majukwaa ya jamii yanayotumiwa na wateja pamoja na wawakilishi wa serikali. Kwa mfano, wakati mnara mpya unajengwa, jamii husika inaweza kuwa na wasiwasi juu ya athari kwa mazingira, jukwaa hili linatupa fursa ya kueleza na kuondoa wasiwasi huo.

**Mfano halisi**

### Juhudi zetu za kuwaelimisha na kuwawezesha wateja wetu kupambana na utapeli

Tuliratibu Wiki ya Kimataifa ya Kujenga Uelewa Dhidi ya Utapeli mwaka huu. Tuliwashirikisha wadhibiti wetu ili kubaini maeneo yenye matukio mengi ya utapeli nchini kote. Timu zetu zilitembelea masoko yetu makuu kote nchini Tanzania na kuwasiliana na wateja ili kubadilishana mawazo kuhusu jinsi ya kulinda taarifa binafsi na kuripoti utapeli. Kwa kuzingatia ushirikiano wetu wa kimkakati na vituo vya redio nchini, tulizindua mpango wa Epuka Utapeli - mfululizo wa hadithi fupi na za kuvutia katika redio za zinazotoa maarifa na uzoefu halisi wa wateja. Pia tulifanya mikutano ya mtandaoni ya VodaChat ili kuongeza uelewa juu ya mbinu mbalimbali za utapeli na jinsi ya kujibu na kuripoti vitendo vya utapeli.

**192 228**
Idadi ya watu
waliofikiwa kupitia Instagram, Facebook, na X

**2 200**
Idadi ya watu
waliofikiwa wakati wa ziara katika miji iliyobainishwa kama maeneo yenye vitendo vingi vya utapeli

Katika siku za usoni, tunapanga kuibadilisha kampeni hii ya uhamasishaji dhidi ya utapeli kuwa endelevu ya muda wote badala ya kuwa ya mara moja kila mwaka.



## Kuwaendeleza wafanyakazi wetu

Tunaamini kwamba ustawi wa wafanyakazi wetu unachangia moja kwa moja katika uwezo wetu wa kutimiza azma yetu ya kuiunganisha jamii kwa kesho iliyobora.

- Tuliboresha thamani ya mafao ya wafanyakazi wetu kupitia sera na taratibu za kujali na jumuishi, ili kujenga utamaduni wa mahali pa kazi unaowawezesha wafanyakazi kustawi na hivyo kuwaletea matokeo chanya katika malengo yao ya ustawi kitaaluma na kutufanya tuweze kutimiza azma yetu. Mwaka huu tulifanya utaratibu ambapo wafanyakazi wetu waliopenda, waliweza kuwalipia wazazi wao bima ya afya kwa gharama nafuu kiasi, kupitia kwa kampuni ya bima inayotoa huduma ya bima ya afya kwa wafanyakazi wetu.

## Kuendeleza uaminifu inaendelea

Thamani iliyojengwa | Thamani iliyopungua | Thamani endelevu

### Ulinzi wa faragha na taarifa za wateja wetu

Tunalenga kusimamia maendeleo ya kasi ya kiteknolojia, kanuni zinazohusiana na matumizi ya taarifa za wateja, pamoja na changamoto, fursa na hatari zinazoweza kujitokeza. Utaratibu wetu wa kulinda usiri na usalama wa taarifa binafsi za wateja unaunda utamaduni na utendaji thabiti wa ulinzi wa taarifa hizo.

- Tumeimarisha mifumo yetu ya utawala na udhibiti inayohusiana na faragha na taarifa za wateja wetu. Tunatumia mifumo ya ufuatiliaji yenye akili mnemba inayotekelezwa kulingana na misingi kutoka kampuni yetu mama ya Kundi la Vodacom. Pia tumeboresha taarifa yetu ya usiri kuonesha kwamba taarifa za wateja wetu zitatumika katika mifumo yetu ya uchambuzi wa takwimu. Hii inaonesha kwamba tumejikita katika matumizi sahihi ya mifumo hiyo huku tukihakikisha kufuatwa kwa sheria za ulinzi wa taarifa za wateja wetu na udhibiti wa mifumo yetu ya kiusalama.

- Vodacom Tanzania ilikuwa miongoni mwa taasisi za kwanza kupokea Hati ya Usajili wa Mchakata na Mdhibiti Taarifa katika hafla ya uzinduzi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Kutambuliwa huku ni ushahidi wa umakini katika kutekeleza ahadi yetu thabiti ya kulinda faragha za wateja wetu kadiri ta matakwa ya kisheria.

- Mikakati mingine muhimu tulioitekeleza mwaka wa fedha 2025 ni pamoja na uzinduzi wa klabu ya usalama mitandaoni kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuendeleza mpango wetu wa "Bug Bounty". Katika mpango huu, tunawaruhusu wataalamu wa teknolojia kutoka nje ya kampuni yetu, kujaribu kuudukua mtandao wetu na kutupa matokeo yake. Taarifa wanazotupa hutusaidia kuimarisha ulinzi dhidi ya mashambulizi ya kiteknolojia katika mtandao wetu.

- Tuliendeleza programu yetu ya faragha na usiri wa taarifa za wateja katika shughuli za kampuni yetu ya Vodacom ikijumuisha kampuni tanzi ya M-Pesa, kwa mujibu wa sera zetu za ndani na udhibiti wa faragha, pamoja na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Tanzania (PDPA). Pia, tuliendesha mafunzo ya ndani kuwaelimisha wafanyakazi wetu kuhusu matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPA), ambayo ilianza kutumika mwezi Aprili 2024.

### Kuilinda jamii

- Popote tunapotenda kazi, tunaweza kuchangia kuendeleza haki za msingi za wateja wetu, wafanyakazi na jamii. Tunatambua uwezekano wa athari zinazohusiana na shughuli zetu na tunafanya kazi kwa bidii kupunguza madhara na kuhakikisha usalama wa jamii.


### Kuhamasisha ununuzi adilifu na jumuishi

- Ili kuhakikisha mazingira ya kazi salama na ya haki na kusimamia ipasavyo masuala ya kimazingira na kijamii katika minyororo yetu ya usambazaji, tunawahimiza wasambazaji na washirika wetu wa kimkakati na kibiashara kuzingatia mbinu za biashara endelevu. Tunakusudia kufanya kazi na wasambazaji ambao wanaendana kwa karibu na malengo yetu na wanaozingatia maadili. Tunatarajia wasambazaji wetu watatimiza viwango vyetu vya msingi vya maadili, ajira na mazingira, na kuwajibika katika kusimamia athari zinazoweza kutokea katika shughuli zao, na pia kuwasimamia wasambazaji wao kwa kiwango cha juu.

- Mwaka huu, tumeendelea kuwawezesha wasambazaji wa ndani ambapo, asilimia 77.0% ya thamani ya manunuzi yetu yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 717.3, yalifanyika kupitia kwa wauzaji 327 wanaoendesha shughuli zao nchini Tanzania.

| Viashiria vya uendelevu wa biashara | Kipimo | Machi-25 | Machi-24 | Machi-23 | Machi-22 | Machi-21 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya wafanyakazi | Idadi | **623** | 607 | 581 | 560 | 569 |
| Idadi ya wafanyakazi wanawake | Idadi | **241** | 231 | 218 | 209 | 203 |
| Wanawake kwenye Kamati ya Uongozi (ExCo) | % | **41.7** | 38.5 | 38.5 | 38.5 | 36.4 |
| Wanawake kwenye menejimenti (wakuu wa vitengo na ExCo) | % | **47.1** | 46.7 | 43.8 | 40.0 | 41.2 |
| Wafanyakazi wanawake | % | **38.7** | 38.1 | 37.5 | 37.3 | 35.7 |
| Jumla ya gharama zilizotumika kugharimia wafanyakazi | (Shilingi bilioni) | **90.4** | 74.7 | 65.2 | 63.8 | 74.7 |
| Jumla ya matumizi katika mafunzo | (Shilingi bilioni) | **1.9** | 1.7 | 0.3 | 0.2 | 0.7 |
| Vifo wakati wa kazi | idadi | **Zero** | Zero | Zero | Zero | Zero |
| Uwajibikaji kwa Bidhaa na Huduma (Customer NPS) | Nafasi | **1st** | 1st | 1st | 1st | 1st |
| Kiwango cha kuridhika cha ushikishwaji wafanyakazi | % | **96** | 94 | 93 | 85 | 86 |
| Wateja wote (siku 90)* | Idadi ('000) | **22 642** | 19 563 | 16 735 | 15 368 | 14 861 |
| Wateja wa M-Pesa (kwa mwezi)* | Idadi ('000) | **11 519** | 10 169 | 8 197 | 6 833 | 7 395 |
| Wateja wa data (kwa mwezi)* | Idadi ('000) | **11 977** | 10 065 | 8 748 | 7 603 | 7 695 |
| Gharama ya uwekezaji | (Shilingi bilioni) | **175.0** | 170.1 | 156.0 | 174.0 | 122.4 |
| Jumla ya kodi na makato yaliyolipwa serikalini | (Shilingi bilioni) | **621.3** | 522.6 | 530.0 | 516.9 | 429.7 |
| Jumla ya mikopo ya muda wa hewani kwa wateja | (Shilingi bilioni) | **131.1** | 101.7 | 87.8 | 68.4 | 43.3 |
| Jumla ya thamani ya miamala iliyopita kwenye M-Pesa | (Shilingi bilioni) | **129.9** | 97.1 | 70.4 | 61.9 | 69.2 |
| Minara vijijini (UCSAF) | Idadi | **422** | 313 | 302 | 283 | 260 |
| % ya wateja wetu walioko vijijini[1] | % | **52.9** | 45.9 | 45.9 | 45.7 | 45.2 |
| Matumizi ya karatasi yaliyoepukwa kwa kutumia vocha za kielektroniki[2] | Tani | **242** | 214 | 172 | 134 | 140 |
| Matumizi ya plastiki yaliyoepukwa kwa kutumia laini – SIM-kadi ndogo[3] | Tani | **34** | 28 | 33 | 21 | 22 |

* Takwimu zote zinazohusu idadi ya wateja, ni kwa mujibu wa kanuni ya tafsiri ya mteja ya kundi la makampuni la Vodacom, isipokuwa ikiwa imeelekezwa vingine.
1. Tumefanya mabadiliko katika asilimia ya wateja katika maeneo ya vijijini ili kuakisi uainishaji wa sasa wa maeneo.
2. Makadirio haya ni iwapo kama miamala yote ya kielektroniki ingefanyika kwa kutumia vocha yetu ya karatasi inayouzwa zaidi.
3. Takwimu za mwaka uliopita zimebadilika ili ziendane na utaratibu wa sasa wa kukokotoa takwimu hii kwa kundi la makamouni ya Vodacom.





# Taarifa ya Mkurugenzi wa Fedha

Hilda Bujiku, Mkurugenzi wa Fedha

Wapendwa wadau wetu, najivunia kuwasilisha matokeo mazuri ya kifedha ya Vodacom Tanzania kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2025.

Licha ya changamoto za mambo ya kisiasa duniani, mkakati wetu unaoongozwa na azma yetu, kasi nzuri kibiashara, na matumizi stahiki ya mtaji wetu unaozingatia thamani, umeleta ukuaji mkubwa wa mapato. Zaidi ya hayo, jitihada zetu za kudhibiti matumizi yetu zimesaidia kuokoa gharama za matumizi, zikisaidia kupunguza athari za changamoto mbalimbali za kiutendaji, ikiwa ni pamoja na ongezeko la gharama lililotokana na ongezeko kubwa la viwango vya kubadilisha fedha za kigeni. Kwa ujumla, tumefanikisha ukuaji imara katika vipimo vyote vya faida na kuboresha kwa kiasi kikubwa faida ya biashara yetu.

## Muhtasari wa taarifa za kifedha

| Shilingi milioni | 2025 | 2024 | % Badiliko la mwaka hadi mwaka |
|---|---|---|---|
| **Mapato ya huduma** | **1 515 987** | **1 258 335** | **20.5** |
| Mapato | **1 539 360** | 1 278 217 | 20.4 |
| **Mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu (EBITDA)** | **493 596** | **394 179** | **25.2** |
| Faida ya uendeshaji | **208 177** | 134 276 | 55.0 |
| Faida baada ya kodi | **90 511** | 53 427 | 69.4 |
| Pato kwa kila hisa (shilingi) | **40.37** | 23.83 | 69.4 |
| Uwiano wa mapato na gharama za moja kwa moja (%) | **67.6** | 67.2 | +0.4ppts |
| Uwiano wa mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu (%) | **32.1** | 30.8 | +1.3ppts |
| Uwiano wa faida ya uendeshaji (%) | **13.5** | 10.5 | +3.0ppts |
| Uwiano wa faida baada ya kodi (%) | **5.9** | 4.2 | +1.7ppts |

**Katika kuimarisha utendaji wa biashara, tulijikita katika kuleta ufanisi wa matumizi ya rasilimali zetu ili kufanikisha ukuaji endelevu, na kupelekea ongezeko la faida kwa wanahisa wetu.**

| Vipaumbele vyetu | Mafanikio yetu |
|---|---|
| Upanuzi wa wigo wa huduma zetu ili kujenga ukuaji wa mapato endelevu | • Mapato ya huduma yaliongezeka kwa 20.5% hadi shilingi bilioni 1 516<br>• Tumepiga hatua katika kupanua wigo wa vyanzo vya mapato yetu. Mchango wa mapato ya huduma kutoka huduma zetu za kisasa ukiacha huduma asilia[1] ulioongezeka kwa alama za asilimia 4 hadi kufikia 29.1% kutoka 25.1% katika mwaka wa fedha 2024<br>• Tumefanikiwa kupata ukuaji thabiti katika vyanzo vyetu vikuu vya mapato ya huduma, ambapo mapato ya M-Pesa yaliongezeka kwa 29.3% na mapato ya data za simu yaliongezeka kwa 21.6%<br>• Tumepata ongezeko la 8.7% katika mapato ya huduma za simu kwa sauti licha ya ushindani wa bei sokoni |
| Utendaji thabiti ili kukuza faida na mzunguko wa fedha kwenye biashara | • Jitihada za kufanya mabadiliko katika matumizi zimetuwezesha kuokoa matumizi ya shilingi bilioni 59.2<br>• Ongezeko la mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu kwa 25.2% hadi kufikia shilingi bilioni 493. Ukiacha athari za ongezeko la viwango vya kubadilishia fedha za kigeni na gharama za mara moja zisizojirudia, uwiano wa mapato haya kwa mapato ya jumla ulifikia 34.1%, ukiakisi ongezeko la alama 3.3 za asilimia<br>• Ongezeko la faida baada ya kodi kwa 69.4% hadi shilingi bilioni 90.5<br>• Mzunguko wa fedha thabiti wa shilingi bilioni 206.9 (Mwaka wa fedha 2024: shilingi bilioni 123.8) |
| Uwekezaji katika teknolojia na maboresho ya miundombinu ya mtandao ili kuchochea ukuaji wa biashara na utekelezaji wa azma yetu | • Tumewekeza shilingi bilioni 175.0[1] katika miundombinu yetu, sawa na 11.4% ya mapato yetu<br>• Uthabiti wa mtandao uliwezesha ongezeko la takriban 50% katika matumizi ya data kupitia teknolojia ya 4G<br>• Mabadiliko ya matumizi katika mtandao wetu – matumizi ya data kupitia teknolojia ya 4G yameongezeka kwa zaidi ya alama za asilimia 5, na sasa yanazidi 80%<br>• Tulijenga minara 7 ya 5G, minara 471 ya 4G na minara 321 ya 3G<br>• Tumejenga minara 109 maeneo ya vijijini na kufikisha jumla ya minara 422 tuliyoijenga katika maeneo ambayo hayakua na huduma za mawasiliano kwa ushirikiano na serikali toka mwaka 2013<br>• Uongozi thabiti wa kipimo cha wateja kuridhika na ubora wa mtandao wetu (NPS)<br>• Tumepata haki ya kutumia masafa ya 800MHz na 2 600MHz baada ya kuinunua Kampuni ya Smile |
| Gawio endelevu kwa wanahisa wetu, likichochewa na hali nzuri ya Kampuni kifedha | • Pendekezo la gawio la mwaka la shilingi bilioni 45.3 (Mwaka wa fedha 2024: shilingi bilioni 26.7) |
| Maboresho ya matarajio ya ukuaji wa biashara yetu | • Tunaboresha lengo letu la ukuaji wa mapato ya huduma kutoka ukuaji usiozidi 9.9% kuwa kiwango kilicho katika makumi ya asilimia |

1 Huduma zetu za kisasa ni pamoja na huduma za kidijitali, huduma za data majumbani na maofisini, mifumo yetu ya vitu vilivyounganishwa kwenye intaneti (IoT) na mapato ya M-Pesa ukiacha mapato ya kutoa na kutuma pesa.

1 Gharama mbali na gharama za kununua na kuungana na Kampuni nyingine, pamoja na mabadiliko katika wadeni wetu katika uwekezaji wa mali na mitambo.



## Upanuzi wa wigo wa huduma zetu ili kujenga ukuaji wa mapato endelevu

Mwaka huu, **mapato ya huduma** yaliongezeka kwa 20.5% hadi shilingi bilioni 1 516.0 yakichagizwa na kasi yetu nzuri kibiashara ambayo ilipelekea ongezeko la 15.7% la wateja na ukuaji wa wastani wa mapato kwa kila mteja (ARPU) wa 4.3%. Ukuaji mkubwa wa mapato ya huduma zetu za kisasa pamoja na ongezeko la mchango wake katika mapato ya huduma vimekuwa ni jambo la kutia moyo. Huduma hizi za kisasa ni pamoja na huduma za data majumbani na maofisini, huduma za kidijitali, mifumo ya vitu vilivyounganishwa kwenye intaneti (IoT) na M-Pesa (isipokua huduma za kutuma na kutoa fedha). Mweleke huu unaimarisha uthabiti wa mapato yetu ya huduma na uendelevu wa ukuaji wake.

**Mapato ya M-Pesa** yaliongezeka kwa 29.3% hadi shilingi bilioni 590.0 na kuongeza mchango wake kwenye mapato ya huduma kwa alama za asilimia 2.7 na kufikia 38.9%. Ongezeko la mapato lilichochewa na ongezeko la wastani wa mapato kwa kila mteja na ongezeko la wateja, vyote vikiakisi kukua kwa matumizi ya huduma za M-Pesa. Mkakati wetu wa kupanua huduma mpya katika mfumo wa M-Pesa ikiwa ni pamoja na mikopo, bima, akiba na malipo kwa wafanyabiashara, ulizidi kuzaa matunda. Mapato kutokana na huduma hizi yaliongezeka kwa karibu 50% mwaka hadi mwaka, na mchango wake kwa mapato ya M-Pesa unaendelea kuongezeka. Ukuaji wa huduma hizi mpya katika M-Pesa umechangia upanuzi wa wigo wa vyanzo vya mapato yetu na kusaidia kuongeza ushirikishaji wa kifedha.

**Mapato ya data za simu** yaliongezeka kwa 21.6% hadi shilingi bilioni 422.2, yakichangiwa na ongezeko kubwa la wateja wa data na matumizi ya data lililochochewa na matumizi makubwa ya huduma zetu za 4G na 5G. Simu janja katika mtandao zilizidi kuongezeka ikiwa ni matokeo ya utekelezaji mzuri kibiashara, uliowezeshwa na uwekezaji endelevu katika mtandao. Mwaka huu, tulijenga minara 471 ya 4G, tuliongeza uwezo wa minara 286 ya 4G iliyopo, pamoja na kuongeza uwezo wetu wa usafirishaji wa mawasiliano ya ndani na ya kimataifa – kupitia mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na mkongo wa baharini wa kukodisha.

**Mapato ya simu kwa sauti** yaliongezeka kwa 8.7% hadi shilingi bilioni 310.6, yakichagizwa na ongezeko la wateja, na vifurushi vitokanavyo na mifumo yetu ya kuchanganua mienendo ya matumizi ya wateja na huduma zetu kwa wateja zilizoboreshwa. Shinikizo la ushindani wa bei za simu kwa sauti liliendelea katika mwaka huu, jambo lililosababisha kupungua kwa 1.3% katika bei ya wastani kwa dakika, huku matumizi yakiendelea kukua, kutokana na uwekezaji tulioufanya katika mtandao.

**Mapato ya Kidijitali na huduma za ziada** yanayojumuisha mikopo ya muda wa hewani na huduma za ziada (VAS), yaliongezeka kwa 4.1% hadi kufikia shilingi bilioni 40.3. Ongezeko hili lilichangiwa na wigo mpana wa bidhaa zetu za kidigitali na huduma zingine za ziada. Mwaka huu, tuliendelea kujikita katika kurahisisha jinsi wateja wetu wanavyojisajili katika huduma za ziada (VAS), pamoja na kujenga uwazi na udhibiti katika huduma ambazo wateja wamejisajili.

**Mapato ya simu zinazoingia** yaliongezeka kwa 2.7% hadi shilingi bilioni 49.7. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa dakika za maongezi zinazopigwa na kuingia kutoka mitandao mingine, likichochewa na ongezeko la wateja na ushindani. Kwa upande mwingine kukua kwa mapato kulipunguzwa na kushuka kwa bei kwa dakika ya simu zinazoingia kufuatia punguzo la 4.5% katika viwango vya bei ya simu zinazoingia kutoka mitandao mingine kulingana na muongozo wa TCRA.

**Mapato ya data za majumbani na maofisini** yaliongezeka kwa 36.7% hadi shilingi bilioni 42.0, yakichochewa na ongezeko la wateja, huku tukiendelea kutekeleza lengo letu la kuunganisha nyumba na biashara katika huduma za mtandao wetu.

## Utendaji thabiti ili kukuza faida na mzunguko wa fedha kwenye biashara

### Mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu (EBITDA)

Hatua zetu makini za kudhibiti gharama ziliimarisha utendaji mzuri wa mapato, na kupelekea mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu ya shilingi bilioni 493.6, sawa na ongezeko la 25.2%, sawa na uwiano wa 32.1% kwa mapato ya jumla – ambalo ni ongezeko la alama za asilimia 1.3. Tukiondoa athari za hasara zilizotokana na ongezeko kubwa la viwango vya kubadilisha fedha za kigeni na gharama zisizojirudia, mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu yaliongezeka kwa 33.0%, huku uwiano wake kwa mapato ya jumla ukifikia 34.1%, sawa na ongezeko la alama za asilimia 3.3.

Dhamira yetu ya kuongeza ufanisi katika matumizi ilipelekea kuokoa gharama ya shilingi bilioni 59.2, sawa na 3.9% ya mapato ya huduma. Akiba hii ilisaidia kupunguza shinikizo la gharama lililotokana na marekebisho ya mfumuko wa bei kwenye mikataba ya huduma iliyopo, ukuaji wa biashara, na hasara kubwa zilizotokana na ongezeko kubwa la viwango vya kubadilisha fedha za kigeni hasa katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha.

Gharama za moja kwa moja zilielekezwa zaidi katika kukuza na kuimarisha njia zetu za usambazaji – ili kuvutia wateja wapya pamoja na kupanua mfumo wa malipo ya wafanyabiashara, huku tukiendelea kudhibiti matumizi yetu. Hivyo, gharama za moja kwa moja ziliongezeka kwa 16.6% hadi kufikia shilingi bilioni 487.4 huku kiwango cha ukuaji gharama kikiwa ni kidogo kuliko kiwango cha ukuaji wa mapato ya huduma, na uwiano wake na mapato ya jumla ukipungua kwa alama za asilimia 0.4 kutokana na mbinu mbalimbali za kudhibiti matumizi.

Gharama za uendeshaji, zilielekezwa zaidi katika kuboresha huduma kwa wateja kupitia upanuzi wa wigo wa mtandao wetu, kuongeza uwezo wa mtandao na rasilimali za kusaidia ukuaji wa biashara. Pia tuliwekeza katika kuongeza uwezo wetu wa usafirishaji wa mawasiliano ya kimataifa kupitia mkongo wa baharini wa kukodisha ili kuongeza ufanisi wa mtandao wetu. Gharama za uendeshaji ziliongezeka kwa 17.6% hadi shilingi bilioni 546.3. Tukiondoa hasara zilizotokana na ongezeko kubwa la viwango vya kubadilisha fedha za kigeni na gharama zisizojirudia, gharama za uendeshaji ziliongezeka kwa 12.9%.

### Faida baada ya kodi

Tulizalisha faida baada ya kodi ya shilingi bilioni 90.5 ikiakisi ongezeko zuri la 69.4%. Tukiondoa hasara zilizotokana na ongezeko kubwa la viwango vya kubadilisha fedha za kigeni na gharama zisizojirudia, faida baada ya kodi iliongezeka kwa 109.6%. Pia, uwiano kati ya faida baada ya kodi na mapato yetu ya jumla uliongezeka hadi kufikia 7.3% - sawa na ongezeko la alama 3.1 za asilimia. Maendeleo haya ya ukuaji wa faida yalichangiwa na ongezeko zuri la mapato ya huduma na msisitizo wetu endelevu wa kudhibiti gharama za matumizi.

### Mzunguko wa fedha

| | 2025 | 2024 | % Badiliko la mwaka hadi mwaka |
|---|---|---|---|
| Mzunguko wa fedha huru za uendeshaji | **206 918** | 123 819 | 67.1 |
| Mzunguko wa fedha huru | **195 423** | 95 740 | 104.1 |
| Gharama za uwekezaji | **174 995** | 170 134 | 2.9 |
| Deni ghafi | **(425 375)** | (183 288) | (132.1) |
| Uwiano wa deni ghafi na mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu | **0.9** | 0.5 | (0.4) |

Mzunguko wetu wa fedha huru za uendeshaji (Operating Free cash flow) wa shilingi bilioni 206.9, unaakisi ongezeko la 67.1%, lililochagizwa na ongezeko la mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu kufuatia matokeo thabiti kibiashara na usimamizi bora wa rasilimali za kuendesha biashara. Pia, tuliwekeza shilingi bilioni 175.0 katika miundombinu yetu, huku kiasi cha shilingi bilioni 146.2 kikitumika kulipia gharama za kodi (pango) za minara ya mawasiliano.

Mzunguko wa fedha huru (Free cash flow), unaojumuisha riba ya fedha taslimu, kodi, gawio tulilolipokea kutoka kwa kampuni tanzu na tulilolipa kwa wanahisa wetu, ulikuwa shilingi bilioni 195.4, sawa na ongezeko la 104.1% ukilinganisha na mwaka uliopita. Ukuaji huu ulitokana hasa na kuongezeka kwa mzunguko wa fedha huru za uendeshaji na kukua kwa mapato ya riba kufuatia ongezeko la riba inayolipwa katika amana zetu za kifedha zilizopo benki baada ya makubaliano yetu na benki husika. Aidha, gharama za riba zilishuka ikilinganishwa na mwaka uliopita ambao ulikuwa na gharama za riba isiyojirudia iliyotokana na mikataba ya kubadilisha fedha za kigeni. Ongezeko la fedha tulizozalisha, kwa sehemu lilipunguzwa na ongezeko la 50.1% la kodi tuliyolipa kadri ya faida ya biashara.

Uimara wa mzunguko wetu wa fedha huru (free cash flow) ulisaidia katika kudhibiti kiwango chetu cha udeni cha 0.9x (uwiano wa deni ghafi na mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu), licha ya ongezeko la deni letu kwa ujumla kwa hasara kutokana na kurekodiwa kwa deni la pango la shilingi bilioni 319.6. Hii ilitokana na matarajio ya kuhuishwa kwa mikataba ya pango ya minara kulingana na masharti ya mkataba na utaratibu wa sera yetu ya uhasibu. Deni ghafi pia liliathiriwa na malipo yasiyojirudia yaliyofanyika kwa ajili ya ununuzi wa kampuni ya Smile Communication Tanzania Limited.

## Uwekezaji katika teknolojia na maboresho ya miundombinu ya mtandao ili kuchochea ukuaji wa biashara na utekelezaji wa azma yetu

Mwaka huu, tuliwekeza shilingi bilioni 175.0 katika miundombinu yetu1, sawa na 11.4% ya mapato, ambazo zilielekezwa katika kuongeza wigo na uwezo wa mtandao wa data pamoja na, kuboresha miundombinu ya TEHAMA. Tuliongeza minara mipya 471 ya 4G na kuimarisha uwezo katika minara 286 ya zamani ya 4G , kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa mtandao wa data kwa teknolojia ya 4G na kuboresha huduma kwa wateja. Uwekezaji huu ulichangia ongezeko la matumizi ya data kwenye mtandao wetu wa 4G ambao uliweza kubeba zaidi ya 80% ya matumizi yote ya data katika mtandao wetu,kitu ambacho kinaenda sambamba na mikakati yetu yenye lengo la kuongeza matumizi ya mtandao wa 4G.

1 Gharama mbali na gharama za kununua na kuungana na Kampuni nyingine, pamoja na mabadiliko katika wadeni wetu katika uwekezaji wa mali na mitambo.

## Maboresho ya matarajio ya ukuaji wa biashara yetu

Kwa kuzingatia vichocheo vya ukuaji wa biashara yetu, utekelezaji wa kimkakati na mazingira ya biashara, tunafurahi kuboresha matarajio yetu ya ukuaji wa mapato ya huduma kutoka kiwango kisichozidi 9.9% kuwa kiwango cha makumi ya asimilia. Sehemu ya mapato itakayowekezwa kwenye miundombinu yetu itabaki kuwa kati ya 13% hadi 16%. Malengo haya ya muda wa kati yatafikiwa iwapo patakuwa na uimara wa shilingi, mazingira ya kisheria na hali ya uchumi kwa ujumla. Malengo haya ni wastani wa kipindi cha miaka mitatu ijayo, bila kujumuisha ununuzi wa masafa, mambo ya kipekee, na shughuli zozote za muunganiko au ununuzi wa kampuni.

## Gawio endelevu kwa wanahisa wetu, linalochochewa na hali nzuri ya Kampuni kifedha

Sera yetu ya gawio inaainisha malipo ya walau 50% ya faida baada ya kodi kama gawio kwa wanahisa kwa mwaka husika. Kwa kuzingatia utendaji wetu mzuri, tumependekeza kwa Bodi kuwaomba kuidhinisha gawio la mwaka la shilingi bilioni 45.3 (Mwaka wa fedha 2024: shilingi bilioni 26.7).

## Shukrani

Mwaka wa fedha 2025 unahitimisha mpango wetu wa miaka mitano chini ya Dira ya 2025 iliyoanza mwaka wa fedha 2021, na kufungua njia kwa Dira ya 2030, itakayotumika kuanzia kipindi cha mwaka wa fedha 2026 hadi 2030.

Ninajivunia mafanikio tuliyoyapata katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Licha ya changamoto za kiuchumi zinazoendelea, ikiwemo ongezeko kubwa la viwango vya kubadilishia fedha za kigeni, matokeo yetu yameonyesha uimara wa mkakati wetu, dhamira yetu kwa wadau wetu, na nguvu ya utekelezaji wetu usioyumba.

Tumefanikiwa kukabiliana na changamoto na fursa mbalimbali ili kuendeleza na kukuza biashara. Katika kipindi hiki, tumeshuhudia ukuaji wa mapato ya huduma kutoka shilingi trilioni moja hadi trilioni moja na nusu. Pia, tumechangia katika ukuaji wa zaidi ya mara mbili wa faida yetu ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020.

Ninawashukuru kwa dhati wafanyakazi wenzangu kwa juhudi zao katika kutimiza lengo letu hili kwa pamoja. Mafanikio haya yalihitaji kujitoa kwa dhati, na sasa kila tunapokumbuka maamuzi na juhudi tulizoweka, tunajivunia kwamba yamepelekea ukuaji mkubwa wa faida kwa wanahisa na kusonga mbele kuelekea azma yetu ya kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora.

Tuna wigo mpana wa huduma na bidhaa zetu, wafanyakazi wenye ujuzi wa hali ya juu mazingira tulivu ya biashara. Hizi ni nyenzo adhimu, tuzitumie kuikuza biashara yetu kuelekea hatua inayofuata na kutimiza matarajio ya wadau wetu.



**Hilda Bujiku**
15 Julai 20255

# Muhtasari wa taarifa za pamoja za hali ya kifedha

| Shm | | Zimekaguliwa 2025 | Zimekaguliwa 2024 |
|---|---|---|---|
| **Mali** | | | |
| **Mali za kudumu** | | **1 573 432** | 1 268 668 |
| Thamani isiyoshikika ya uwekezaji | | **1 639** | 1 639 |
| Mali na mitambo | 1 | **553 807** | 595 659 |
| Mali zisizoshikika | 2 | **298 042** | 280 069 |
| Haki ya matumizi ya mali | 3 | **586 593** | 270 992 |
| Malipo ya 'Haki ya matumizi' kabla ya kutumia | 4 | **56 869** | 29 159 |
| Madeni ya kibiashara na madeni mengine | | **9 882** | 12 800 |
| Kodi ya mapato inayotarajiwa kurejeshwa | | **34 298** | 36 120 |
| Kodi iliyoahirishwa | 5 | **31 206** | 42 230 |
| Uwekezaji mwingine | | **1 096** | – |
| **Mali za muda mfupi** | | **1 404 542** | 1 107 067 |
| Malipo ya 'Haki ya matumizi' kabla ya kutumia | | **15 446** | 12 756 |
| Mali ghalani | | **4 300** | 3 409 |
| Madeni ya kibiashara na madeni mengine ya kulipwa | 6 | **124 396** | 114 380 |
| Ruzuku kutoka serikalini inayotarajiwa kupokelewa | 7 | **13 283** | – |
| Kodi ya mapato inayotarajiwa kurejeshwa | | **25 415** | 24 532 |
| Rasilimali za kifedha – M-Pesa | 8 | **923 235** | 730 293 |
| Fedha taslimu na mbadala wa fedha | 9 | **298 467** | 221 697 |
| **Jumla ya mali** | | **2 977 974** | 2 375 735 |
| **Mtaji na Madeni** | | | |
| **Akiba ya mtaji** | | | |
| Mtaji wa hisa | | **112 000** | 112 000 |
| Malipo ziada kwenye hisa | | **442 435** | 442 435 |
| Mchango wa mtaji | | **27 698** | 27 698 |
| Ziada ya faida iliyotunzwa | 10 | **334 371** | 270 660 |
| Mtaji stahiki kwa wamiliki wa kampuni | | **916 504** | 852 793 |
| Stahiki ya wenyehisa chache | | **75** | 41 |
| **Jumla ya mtaji** | | **916 579** | 852 834 |
| **Madeni ya muda mrefu** | | **642 348** | 297 883 |
| Madeni ya pango | 11 | **620 544** | 281 831 |
| Madeni mengine ya kifedha | | **13 831** | 9 292 |
| Tahadhari ya madeni | | **7 973** | 6 760 |
| **Madeni ya muda mfupi** | | **1 419 047** | 1 225 018 |
| Madeni ya pango | 12 | **84 703** | 110 931 |
| Madeni mengine ya kifedha | | **4 764** | 2 930 |
| Ruzuku za serikali | | **852** | 735 |
| Kodi ya mapato inayotarajiwa kulipwa | | **2 576** | – |
| Madeni ya biashara yanayohusu M-Pesa | 13 | **923 235** | 730 293 |
| Madeni ya biashara na mengine ya kulipa | 14 | **396 929** | 374 540 |
| Malipo ya gawio | | **277** | 269 |
| Tahadhari ya madeni | | **5 711** | 5 320 |
| **Jumla ya madeni** | | **2 061 395** | 1 522 901 |
| **Jumla ya madeni na mtaji** | | **2 977 974** | 2 375 735 |

1. Upungufu umetokana na ongezeko la gharama za uchakavu ambao limepunguza ongezeko lililotokana na uwekezaji uliofanyika mwaka huu.
2. Mali zisizoshikika ziliongezeka kwa 6.4%, ambapo ongezeko la mali mpya lilifidia ongezeko la kila mwaka la gharama za uchakavu. Tumeongeza leseni mpya na kuboresha leseni zilizopo kwa ajili ya mtandao na majukwaa yetu, ili kuimarisha ufanisi wa mtandao sambamba na ukuaji wa biashara. Pia jambo hili litasaidia kuongeza uimara, usalama, na kuwezesha upatikanaji wa haraka huko baadaye wa leseni za mtumizi mapya ikiwemo maboresho ya programu za kiteknolojia.
3. Katika mwaka huu wa fedha, haki ya matumizi ya rasilimali ya shilingi bilioni 319.6 iliongezwa kulingana na masharti ya mikataba ya ukodishaji wa sehemu ya minara na pango na sera za uhasibu. Uwekezaji huu wa ziada ulipunguzwa kwa sehemu na gharama za uchakavu za kila mwaka.
4. Ongezeko hili linatokana hasa na malipo ya awali kwa ajili ya haki ya matumizi ya miundombinu ya mkongo wa mawasiliano, ambapo kwa sehemu ilipunguzwa na gharama za uchakavu za kila mwaka.
5. Upungufu huu unatokana hasa na matumizi ya haraka ya hasara za kodi zilizobebwa kutoka miaka ya nyuma, kufuatia ongezeko la faida ya biashara. Hata hivyo, sehemu ya upungufu huo ilifidiwa na kurekodiwa kwa ongezeko la unafuu wa kodi wa baadae kutokana na tofauti za muda na tofauti za kudumu katika kukokotoa faida ya kikodi.
6. Ongezeko hili limesababishwa hasa na malipo ya awali kwa ajili ya bima ya mali na salio la amana za wateja wa M-Pesa, madeni wanayodaiwa wateja kutokana na mikopo ya nipige tafu na wateja tulioingia nao mikataba ya kibiashara, sambamba na ukuaji wa biashara. Ukuaji huu kwa sehemu ulipunguzwa na hasara za mikopo zinazotarajiwa kulingana na sera za kampuni.
7. Salio hili linawakilisha kiasi kinachotarajiwa kupokelewa kama ruzuku kutoka serikalini kupitia Mfuko wa Upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), kwa ajili ya ujenzi wa minara 147.
8. Ongezeko hili linatokana hasa na amana kutoka kwa wateja na mawakala wa M-Pesa, likiakisi ukuaji endelevu wa biashara ya M-Pesa.
9. Ongezeko hili limesababishwa hasa na ongezeko la fedha taslimu kutokana na shughuli za biashara. Kwa sehemu, fedha hizo zilitumika katika shughuli za uwekezaji na mtaji, ikijumuisha malipo ya pango ya ukodishaji wa minara, pamoja na malipo ya riba kwa wateja wa M-Pesa. Ongezeko hili lilipunguzwa kwa kiasi na hasara ya kiasi cha shilingi billion 2.9 iliyotokana na ongezeko la viwango vya kubadilisha fedha za kigeni.
10. Ongezeko hili limesababishwa hasa na faida iliyopatikana katika mwaka wa fedha, ambapo kwa kiasi lilipunguzwa na malipo ya gawio la shilingi bilioni 26.6 lililotangazwa na kulipwa kwa ajili ya mwaka wa fedha 2024.
11. Ongezeko hili linatokana hasa na kuhuishwa kwa mikataba ya ukodishaji wa minara kulingana na masharti ya mikataba hiyo na sera yetu ya uhasibu. Uwekezaji huu wa ziada ulipunguzwa kwa kiasi na malipo yaliyofanyika kwa mikataba ya ukodishaji iliyoivа.
12. Upungufu huu umetokana hasa na tofauti za muda kati ya malipo ya ukodishaji wa sehemu ya minara na pango, pamoja na uainishaji wa deni la muda mrefu kuwa deni la mikataba ya ukodishaji ya muda mfupi.
13. Ongezeko hili linatokana hasa na amana kutoka kwa wateja na mawakala wa M-Pesa, likiakisi ukuaji endelevu wa biashara ya M-Pesa.
14. Ongezeko hilo limesababishwa hasa na ongezeko la kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na ushuru wa forodha kutokana na ukuaji wa mapato, ongezeko la riba ya M-Pesa inayolipwa kwa wateja, na malimbikizo ya nyuma ya gharama za TEHAMA na mtandao. Ongezeko hili kwa sehemu lilipunguzwa baada ya malipo ya ununuzi wa kampuni ya Smile Communications Tanzania Limited mwishoni mwa mwaka wa fedha 2024.

# Muhtasari wa taarifa za pamoja za mzunguko wa fedha

| Shm | | Zimekaguliwa 2025 | Zimekaguliwa 2024 |
|---|---|---|---|
| **Mzunguko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji** | 1 | **718 714** | 643 087 |
| Malipo ya kodi ya mapato | | **(39 860)** | (26 549) |
| **Mzunguko ghafi wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji** | | **678 854** | 616 538 |
| **Mzunguko wa fedha zilizotumika katika shughuli za uwekezaji** | | | |
| Nyongeza katika mali na mitambo, na mali zisizoshikika | | **(198 019)** | (179 916) |
| Mali zilizonunuliwa | 2 | **(60 720)** | (12 501) |
| Ununuzi wa uwekezaji mwingine | 3 | **(1 096)** | – |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali na mitambo | | **–** | 419 |
| Ruzuku za serikali zilizopokelewa | 4 | **2 955** | 14 456 |
| Mapato ya fedha yaliyopokelewa | | **7 169** | 4 409 |
| Ongezeko la fedha zilizowekwa kwenye akiba za matumizi maalum | 5 | **(192 942)** | (220 935) |
| Riba kutoka amana za M-Pesa | | **38 947** | 21 355 |
| **Mzunguko halisi wa fedha katika shughuli za uwekezaji** | | **(403 706)** | (372 713) |
| **Mzunguko wa fedha kutokana na shughuli za ugharimiaji** | | | |
| Gawio lililolipwa | 6 | **(26 758)** | (22 265) |
| Riba ya madeni ya pango iliyolipwa | 7 | **(53 901)** | (47 774) |
| Gharama ya kinga ya kukabiliana na athari za kushuka kwa thamani ya shilingi | | **(875)** | (5 767) |
| Mkopo wa muda mfupi | | **–** | 47 266 |
| Rejesho la mkopo wa muda mfupi – mtaji | | **–** | (47 266) |
| Rejesho la riba ya mkopo wa muda mfupi | | **–** | (1 312) |
| Rejesho la madeni mengineyo – mtaji | | **(4 762)** | (771) |
| Rejesho la riba la madeni mengineyo | | **(386)** | (280) |
| Riba iliyolipwa kwa wateja wa M-Pesa | | **(16 493)** | (19 596) |
| Rejesho la deni la leseni ya masafa yaliyonunuliwa | | **–** | (75 465) |
| Rejesho la riba ya deni ya leseni ya masafa yaliyonunuliwa | | **–** | (1 925) |
| Malipo ya madeni ya pango – mtaji | | **(92 312)** | (87 070) |
| **Mzunguko halisi wa fedha zilizotumiwa katika shughuli za ugharimiaji** | | **(195 487)** | (262 225) |
| **Punguzo ghafi katika fedha na fedha mbadala** | | **79 661** | (18 400) |
| **Fedha taslimu na fedha mbadala mwanzoni mwa mwaka wa fedha** | | **221 697** | 236 590 |
| Athari za mabadiliko ya viwango vya kubadili fedha katika fedha taslimu na fedha mbadala zilizo katika fedha za kigeni | | **(2 891)** | 3 507 |
| **Fedha taslimu na fedha mbadala mwisho wa mwaka** | | **298 467** | 221 697 |

1. Ongezeko hilo limetokana na utendaji bora wa biashara na makusanyo mazuri kutoka kwa wateja, hali kwa sehemu likipunguzwa na malipo kwa wasambazaji na wauzaji wetu.
2. Ongezeko hili linaakisi uwekezaji endelevu katika kuongeza wigo na uwezo wa mtandao wa data pamoja na, kuboresha miundombinu ya TEHAMA.
3. Hili linawakilisha malipo kwa wanahisa wa Smile Holdings kufuatia ununuzi wa kampuni ya Smile Communications Tanzania Limited uliokamilika mwishoni mwa mwaka wa fedha 2024.
4. Malipo haya yanahusiana na malipo ya awamu yaliyopokelewa kutoka Mfuko wa Upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano kwa Wote kama ruzuku ya kusaidia ujenzi wa minara mipya katika maeneo yasiyokuwa na huduma za mawasiliano pamoja na, kuboresha minara ya 2G na 3G iliyopo kuwa 4G.
5. Upungufu huu ulitokana na M-Pesa ambayo haijalipwa kwa wateja na mawakala, yakingojea idhini ya mdhibiti.
6. Hii inahusiana na gawio la faida lililotangazwa na kulipwa kwa wanahisa kwa mwaka wa fedha 2024,pia ikijumuisha malipo ya sehemu ya gawio la miaka ya nyuma ambayo yalisalia.
7. Inahusiana na malipo ya riba kwa mikataba ya ukodishaji wa sehemu ya minara na pango, ambapo ongezeko limesababishwa hasa na mikataba mipya iliyosainiwa mwaka huu.







# Taarifa ya mkutano mkuu

**Vodacom Tanzania Public Limited Company**
(Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
(Namba ya usajili 38501)
(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)
('Vodacom Tanzania' au 'Kampuni')

**Taarifa inatolewa kuwa, mkutano mkuu wa tisa wa Kampuni kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2025 utafanyika kwa njia ya kielektroniki siku ya Alhamisi tarehe 21 Agosti 2025 kuanzia saa nne asubuhi. Mkutano huu utajadili yafuatayo:**

## 1. Kuthibitisha kumbukumbu

Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa nane uliofanyika tarehe 11 Septemba 2024.

**Azimio la kawaida namba 1**

"ILIAMULIWA KUWA kumbukumbu za mkutano mkuu wa nane uliofanyika tarehe 11 Septemba 2024 zimethibitishwa."

Nakala za kumbukumbu zinapatikana kwenye tovuti ya Kampuni **www.vodacom.co.tz/annual-general-meeting**.

## 2. Kupitisha taarifa za fedha za mwaka zilizokaguliwa

Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2025.

**Azimio la kawaida namba 2**

"ILIAMULIWA KUWA taarifa za fedha zilizokaguliwa za Kampuni, pamoja na ripoti ya wakaguzi huru na ya wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2025, zimepokelewa na kupitishwa."

Nakala za taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2025 zinapatikana katika tovuti ya Kampuni **www.vodacom.co.tz/financials**.

## 3. Uchaguzi wa wakurugenzi

Kwa kupitia maazimio tofauti:

3.1 Bw David Tarimo aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru kwa mujibu wa ibara ya 86 ya Katiba ya Kampuni, kujaza nafasi iliyojitokeza katika Bodi na kuendelea kutekeleza majukumu ya kiofisi hadi mkutano wa kawaida unaofuata, na hivyo anastahili kuchaguliwa.

3.2 Bw Mohamed Abdallah aliteuliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji kwa mujibu wa ibara ya 86 ya Katiba ya Kampuni, kujaza nafasi iliyojitokeza katika Bodi na kuendelea kutekeleza majukumu ya kiofisi hadi mkutano wa kawaida unaofuata, na hivyo anastahili kuchaguliwa.

3.3 Bi Margaret Ikongo, Bi Kanini Mutooni na Bi Hilda Bujiku wanastahili kustaafu katika mkutano huu kwa mujibu wa ibara 104 na 105 za Katiba ya Kampuni. Ibara hizo zinabainisha kuwa licha ya kustaafu, wanaweza kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa wakurugenzi.

**Azimio la kawaida namba 3**

"ILIAMULIWA KUWA Bw David Tarimo amechaguliwa kuwa mkurugenzi huru."

**Azimio la kawaida namba 4**

"ILIAMULIWA KUWA Bw Mohamed Abdallah amechaguliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

**Azimio la kawaida namba 5**

"ILIAMULIWA KUWA Bi Margaret Ikongo amechaguliwa kuwa mkurugenzi huru."

**Azimio la kawaida namba 6**

"ILIAMULIWA KUWA Bi Kanini Mutooni amechaguliwa kuwa mkurugenzi huru."

**Azimio la kawaida namba 7**

"ILIAMULIWA KUWA Bi Hilda Bujiku amechaguliwa kuwa mkurugenzi mtendaji."

## Taarifa ya mkutano mkuu inaendelea

### 4. Uteuzi wa Ernst & Young kuwa wakaguzi huru wa Kampuni

Kuteua kampuni ya Ernst & Young Inc., kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji, kuwa wakaguzi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mkutano mkuu ujao wa mwaka.

#### Azimio la kawaida namba 8

"ILIAMULIWA KUWA Ernst & Young Inc. imeteuliwa kuwa mkaguzi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mkutano mkuu ujao wa mwaka."

### 5. Uteuzi wa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji

Kupitia maazimio tofauti na kwa mujibu wa kifungu cha 32(f) cha Katiba ya Kampuni, Bi Margaret Ikongo, Bi Thembeka Semane na Bi Kanini Mutooni wakiwa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji wachaguliwe kuendelea kuwa wajumbe.

#### Azimio la kawaida namba 9

"ILIAMULIWA KUWA, kwa kuzingatia idhini ya azimio namba 5, Bi Margaret Ikongo amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

#### Azimio la kawaida namba 10

"ILIAMULIWA KUWA Bi Thembeka Semane amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

#### Azimio la kawaida namba 11

"ILIAMULIWA KUWA, kwa kuzingatia idhini ya azimio namba 6, Bi Kanini Mutooni amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

### 6. Gawio

Kuidhinisha gawio la mwisho la shilingi 20.20 kwa kila hisa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2025 kama ilivyopendekezwa na wakurugenzi. Gawio litalipwa kabla ya au tarehe 15 Oktoba 2025 kwa wanahisa waliosajiliwa kwenye kitabu cha usajili baada ya kufunga biashara ya hisa tarehe 15 Agosti 2025.

#### Azimio la kawaida namba 12

"ILIAMULIWA KUWA gawio la shilingi 20.20 kwa hisa ya kawaida kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2025 limeidhinishwa."

### 7. Ada ya wakurugenzi

Kuidhinisha ada ya wakurugenzi wasio watendaji ya dola za Kimarekani 482 000 hadi hitimisho la mkutano mkuu ujao wa mwaka, ili kuiwezesha Kampuni kuwavutia watu wenye uwezo, ujuzi na uzoefu unaotakiwa ili kutoa mchango unaofaa kwa Kampuni.

Majukumu ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji sasa yameongezeka na kujumuisha usimamizi wa masuala ya kijamii na maadili, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Kanuni Kumi za Mkataba wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa (UN Global Compact) zinazohusu haki za binadamu, ajira, mazingira, na kupambana na rushwa – pamoja na shughuli za uwekezaji katika jamii. Kwa kutambua majukumu haya, ongezeko la malipo ya Mwenyekiti wa Kamati kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 5 000 linapendekezwa.

#### Azimio la kawaida namba 13

"ILIAMULIWA KUWA kiwango cha ada ya mwaka ya wakurugenzi wasio watendaji cha dola za Kimarekani 482 000 kimeidhinishwa kwa mchanganuo ufuatao:

| | Pendekezo la ada Dola ya Marekani[1] | Ada ya sasa Dola ya Marekani |
|---|---|---|
| Mwenyekiti wa Bodi | **150 000** | 150 000 |
| Mjumbe wa Bodi | **30 000** | 30 000 |
| Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | **20 000** | 15 000 |
| Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | **8 000** | 8 000 |
| Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira | **12 000** | 12 000 |
| Mjumbe wa Kamati ya Ujira | **4 000** | 4 000 |
| Mjumbe wa Kamati ya Uteuzi | **3 000** | 3 000 |

1 Ada hii inajumuisha kodi zote ikijumuisha kodi ya zuio, inayolipwa kwa shilingi ya Kitanzania kwa wakurugenzi wazawa, randi ya Afrika Kusini kwa wakurugenzi wa Afrika Kusini na dola ya Marekani kwa wakurugenzi wengine. Ada hii inalipwa kila robo mwaka.

## Wasifu wa Wajumbe wa Bodi

### David Tarimo (61)

Mkurugenzi huru

*Shahada ya Sheria (LLB) ya Heshima, Chuo cha Kings, Chuo Kikuu cha London. Mwanachama wa Taasisi ya Wahasibu Waliosajiliwa nchini Uingereza na Wales (FCA). Mwanachama wa Taasisi ya Ushuru ya Uingereza (CTA).*

David aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru na Mwenyekiti wa Bodi kuanzia Aprili 2025. Hapo awali alihudumu PwC (Tanzania) kwa karibu miongo mitatu, ikiwa ni pamoja na miaka kumi kama Mwanaubia Kiongozi wa Nchi na miaka kumi na minne katika nafasi mbalimbali za uongozi wa kikanda wa masuala ya ushuru ndani ya Kanda ya Afrika ya Kampuni ya PwC. David ana uzoefu wa miongo minne katika masuala ya ushuru, ushauri, na uundaji wa sera katika sekta mbalimbali za uchumi, zikiwemo kilimo, huduma za kifedha, viwanda, madini, mafuta na gesi, mawasiliano, na huduma za jamii. Mchango wake katika sera za umma unajumuisha kuwa mwanachama wa Kikosi Kazi cha Waziri wa Fedha cha kuunda bajeti (tangu 2002), Kamati ya Bomani ya Madini (2008), na Tume ya Rais ya Mageuzi ya Ushuru (2024 hadi sasa). Kwa sasa anahudumu kama Mwenyekiti wa Jukwaa la Wakurugenzi Wakuu wa Makampuni Tanzania (CEO Roundtable of Tanzania).

### Mohamed Abdallah (48)

Mkurugenzi asiye mtendaji

*Shahada ya Biashara, Chuo Kikuu cha Ain Shams, Cairo.*

Mohamed Abdallah ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Vodafone Misri tangu mwaka 2020 na aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu Mtendaji wa Vodacom International Business kuanzia tarehe 1 Aprili 2025. Katika jukumu lake la kikanda kama Afisa Mkuu, Mohamed anaongoza masoko ya kimataifa ya Vodacom barani Afrika ambayo ni: Msumbiji, Tanzania, Lesotho na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), kwa kutumia fursa za ushirikiano na ukuaji katika kila nchi. Uzoefu wake mpana na mafanikio mbalimbali katika taaluma yake ndani ya Vodafone tangu alipojiunga mwaka 1998, umemuwezesha kuwa na rekodi ya mafanikio katika sekta ya mawasiliano. Akiwa na uzoefu wa zaidi ya miongo miwili, ameongoza maeneo muhimu kama vile Masoko ya Biashara, Huduma za Intaneti, Huduma za Ziada Zaidi (VAS) na Maudhui, Masoko kwa Wateja Binafsi na Mauzo kwa Makampuni, ambapo alifanikiwa kuleta ukuaji mkubwa katika ubunifu na kuridhika kwa wateja.

### Hilda Bujiku (46)

Mkurugenzi wa fedha

Mjumbe wa kamati ya Utendaji ya Vodacom Tanzania Plc

*Cheti cha Taaluma ya Uhasibu (CPA) kutoka Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania. Shahada ya Biashara(Uhasibu) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Programu kwa Maafisa wa juu wa Vodacom - Taasisi ya Sayansi ya Biashara ya Gordon, Afrika Kusini.*

Hilda ni Mkurugenzi wa Fedha wa Vodacom Tanzania PLC tangu Januari 2022. Alijiunga na Vodacom Tanzania mwaka 2012 na kushika nyadhifa mbalimbali za juu katika kampuni ikijumuisha Naibu Mkurugenzi wa Fedha anayehusika na Mipango na Uchambuzi wa Fedha, Mahusiano ya Wawekezaji na Sekretarieti ya Kampuni. Baadaye alihamishiwa Lesotho kama Mkurugenzi wa Fedha. Hilda ana uzoefu wa zaidi ya miaka 16 akifanya kazi katika kampuni za mawasiliano ya simu.

### Margaret Ikongo (67)

Mkurugenzi huru

Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii

*Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu Huria, Tanzania. Cheti cha Kimataifa cha Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Taasisi ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Uingereza. Diploma ya Kimataifa ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi na Mjumbe Mhitimu wa Taasisi ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Uingereza. Mwanachama katika Taasisi ya masuala ya Bima, Uingereza.*

Margaret aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Pia ni mjumbe wa bodi ya wakurugenzi ya Actuarial and Risk Consulting na Metrolife and Meticulus Insurance. Kabla ya hapo, Margaret alikaa kwenye Bodi ya benki ya NMB na AAR Insurance Tanzania, pamoja na Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). Margaret ana uzoefu mkubwa katika masuala ya fedha na utawala bora akiwa ameupata kutokana na kufanya kazi katika sekta ya bima ambapo alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Taifa kwa kupindi cha miaka kumi. Margaret pia alikuwa mshauri wa Kamishna wa Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania pamoja na Kaimu Mkuu wa Kurugenzi ya Ufundi.

### Thembeka Semane (49)

Mkurugenzi huru

Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii

*Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Monash Stashahada ya Juu katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Biashara cha Pretoria Gordon Shahada ya Biashara katika Uhasibu; Chuo Kikuu cha Transkei (Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Walter Sisulu kwa sasa) Mwanachama wa Taasisi ya Taaluma ya Benki ya Afrika Kusini.*

Thembeka aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Thembeka ana uzoefu katika masuala ya biashara ukihusisha mikakati ya mashirika, utekelezaji wa mifumo ya biashara, miradi yenye thamani kubwa, utekelezaji na ufuatiliaji, utawala bora na vilevile usimamizi wa fedha. Thembeka ni mkurugenzi wa Linea Consulting (Pty) Ltd, mjumbe wa Kamati ya Udhibiti ya ACASA & ATNS, akiripoti kwa Waziri wa Usafirishaji wa Afrika Kusini na pia, ni mjumbe wa Baraza la ICASA. Thembeka anafanya kazi kama mjumbe wa bodi wa Idara ya Makazi EAAB, ambapo ni Mwenyekiti wa Kamati yake ya Fedha na Uwekezaji na pia, ni mjumbe wa Kamati za Ukaguzi na Dharura pamoja na ya Rasilimali watu na Ujira. Pia, Thembeka ni mjumbe wa bodi na mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Dharura na Kamati ya Ujira ya Mamlaka ya usimamizi wa Mbuga za Wanyama za Afrika Kusini. Vilevile, Thembeka ni mjumbe wa South African Heritage Resource Agency na Kamati ya Uthibiti na Usimamizi wa Utendaji wa Manispaa ya Sol Platje.

### Kanini Mutooni (49)

Mkurugenzi huru

Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii

*Elimu ya utekelezaji wa Sera za Kimataifa, Shule ya masuala ya kiserikali ya Harvard Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Shule ya Biashara Cass ya Chuo Kikuu cha Jiji la London. Diploma ya masuala ya Dhamana (Uingereza) Cheti cha Taaluma ya Usimamizi katika Uwekezaji (Uingereza) Cheti cha Taaluma ya Uhasibu (ACCA), Uingereza Shahada ya Biashara, Chuo Kikuu cha Kikatoliki, Kenya.*

Kanini aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Oktoba 2022. Kanini ni Mkurugenzi Mtendaji wa Draper Richards Kaplan Foundation kwa Afrika. Hivi sasa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Draper Richards Kaplan Foundation akisimamia Afrika. Pia ni mjumbe katika Bodi za Financial Sector Deepening Africa (FSDA); MCE Social Capital, the United Nations Capital

Development Fund, Africa Enterprise Challenge Fund, Amref Health Innovation na CDC UK PLC. Kabla ya hapo, Kanini alikuwa mjumbe wa Bodi katika benki za uwekezaji huko Uingereza na Marekani ikiwa ni pamoja na Bank of America-Merrill Lynch na Dresdner Kleinwort Benson.

## Tarehe ya kufunga rejesta

Tarehe ya kufungwa rejesta ya wanahisa wa Kampuni kwa madhumuni ya kustahili kuhudhuria, kushiriki na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni Jumatano 13 Agosti 2025.

## Ushiriki kwa njia ya kielektroniki

Mkutano mkuu wa mwaka utafanyika kwa njia ya kielektroniki kama ilivyoainishwa kwenye kifungu 29 na 63 cha Katiba ya Kampuni. Wanahisa waliosajiliwa kwenye rejesta hadi kufikia tarehe ya kufunga rejesta hiyo, watapokea ujumbe mfupi wa maneno wenye taarifa za kuwawezesha kuingia kwenye mkutano huo. Mkutano mkuu wa mwaka utaoneshwa mubashara kupitia kiunga cha wavuti kwenye vifaa janja vilivyounganishwa na intaneti. Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya Kampuni **www.vodacom.co.tz/annual-general-meeting**

Wanahisa watawajibika kwa gharama za data na mtandao. Kampuni haitawajibika na upotevu wa mawasiliano kutokana na matatizo ya kimtandao/kuishiwa muda wa hewani/kukatika kwa umeme/na matatizo ya kiufundi ya kielektroniki yanayoweza kuathiri ushiriki wa mwanahisa kwenye mkutano mkuu mwaka kwa njia ya mtandao.

Wanahisa wanahimizwa kutuma maswali yatokanayo na maazimio yaliyopo kwenye taarifa hii kabla ya mkutano mkuu kwenda kwenye barua pepe **investorrelations@vodacom.co.tz** kabla ya Ijumaa ya tarehe 15 Agosti 2025 saa 4:00 asubuhi. Majibu ya maswali hayo yatatolewa katika mkutano mkuu. Uwasilishaji wa maswali haumzuii mwanahisa kuuliza maswali siku ya mkutano mkuu.

## Mahudhurio

Wanaostahili kuhudhuria, kuzungumza na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni wanahisa tu.

Wanahisa wanaweza kuteua wawakilishi kuhudhuria, kutoa maoni na kupiga kura kwa niaba yao. Mwakilishi si lazima awe mwanahisa wa Kampuni. Fomu ya uwakilishi iliyojazwa, inayopatikana kwenye tovuti ya Kampuni, pamoja na risiti ya uwekezaji ya DSE ya mwanahisa, kitambulisho cha taifa/kura/leseni ya udereva na taarifa za mawasiliano vitumwe kwa barua pepe kwenda **investorrelations@vodacom.co.tz** au viwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni, ghorofa ya 7, Vodacom Tower, Ursino Estate, Kiwanja namba 23, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanzania kabla ya saa 4:00 asubuhi Ijumaa ya tarehe 15 Agosti 2025. Kujazwa kwa fomu ya mwakilishi hakumzuii mwanahisa yeyote kuhudhuria mkutano mkuu wa mwaka.

Upigaji kura utaendeshwa kulingana na Katiba na kanuni za Kampuni. Maazimio ya kawaida yatakayopitishwa katika mkutano mkuu huu yatapaswa kuungwa mkono na zaidi ya 50% ya kura za wanahisa. Azimio maalum litapaswa kuungwa mkono na angalau 75% ya kura za wanahisa.

Wanahisa wenye hisa zisizo kwa majina yao lazima wawapatie watunzaji au wawakilishi wao maelekezo ya kupiga kura katika mkutano mkuu wa mwaka. Kama mtunzaji au mwakilishi wako hatapokea maelekezo kutoka kwako, kama itakavyokuwa, itabidi kufanya maamuzi kulingana na mamlaka uliyoyatoa kwake.

Wanahisa wanahimizwa kuendelea kufuatilia tovuti ya Kampuni ili kupata taarifa zaidi zinazohusiana na mkutano mkuu wa mwaka.

Imeidhinishwa na Bodi.

**Caroline M Mduma**
Katibu wa Kampuni
22 Julai 2025





# Fomu ya mwakilishi

**Vodacom Tanzania Public Limited Company**
(Imesajiliwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
(Namba ya Usajili 38501)
(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)
("Vodacom" au "Kampuni")

**Kifungu A** – Ijazwe na wanahisa wote

Jina Kamili

Namba ya hati ya hisa (CDS A/c No) | Idadi ya hisa mwanahisa anazomiliki

**Kifungu B –** Ijazwe na wanahisa watakaoteuwa wawakilishi (na si Mwenyekiti) kuhudhuria mkutano kwa niaba yao

Mimi(Sisi), mwenye/wenye hati ya hisa zenye idadi ya hisa za kampuni kwa mujibu wa kifungu A, namteua/tunamteua (angalia maelekezo namba 1&2)

au akishindwa yeye,

au akishindwa yeye,

**Mwenyekiti** wa mkutano mkuu wa mwaka kuwa mwakilishi wangu/wetu kuhudhuria, kushiriki mijadala na kupiga kura kwa niaba yangu/yetu katika mkutano mkuu wa tisa utakaofanyika kwa nji ya kielektroniki siku ya **Alhamisi, tarehe 21 Agosti 2025** kwa lengo la kutoa maamuzi na kupitisha maazimio ya kawaida, kupiga kura ya kuafiki au kutokuafiki au kutoshiriki kwenye upigaji kura kulingana na hisa zilizoandikishwa kwa jina langu/letu.

**Kifungu C** – Ijazwe na wanahisa wote

Weka alama x kwenye kisanduku kulingana na matakwa yako.
**Vinginevyo mwakilishi wako atapiga kura atakavyoona inafaa.**

| | Naafiki | Siafiki | Sishiriki |
|---|---|---|---|
| 1. **Azimio la kawaida namba 1** Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa mwaka uliofanyika tarehe 11 Septemba 2024 | | | |
| 2. **Azimio la kawaida namba 2** Kupitisha taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2025 | | | |
| 3. **Azimio la kawaida namba 3** Kumchagua David Tarimo kuwa mkurugenzi huru | | | |
| 4. **Azimio la kawaida namba 4** Kumchagua Mohammed Abdallah kuwa mkurugenzi asiye mtendaji | | | |
| 5. **Azimio la kawaida namba 5** Kumchagua tena Margaret Ikongo kuwa mkurugenzi huru | | | |
| 6. **Azimio la kawaida namba 6** Kumchagua tena Kanini Mutooni kuwa mkurugenzi huru | | | |
| 7. **Azimio la kawaida namba 7** Kumchagua tena Hilda Bujiku kuwa mkurugenzi mtendaji | | | |
| 8. **Azimio la kawaida namba 8** Kuchagua Ernst & Young Inc. kuwa wakaguzi wa Kampuni kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2026 | | | |
| 9. **Azimio la kawaida namba 9** Kumchagua tena Margaret Ikongo kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | | |
| 10. **Azimio la kawaida namba 10** Kumchagua tena Thembeka Semane kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | | |
| 11. **Azimio la kawaida namba 11** Kumchagua tena Kanini Mutooni kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | | |
| 12. **Azimio la kawaida namba 12** Kuidhinisha gawio la shilingi 20.20 kwa hisa kwa mwaka ulioishia terehe 31 Machi 2025 | | | |
| 13. **Azimio la kawaida namba 13** Kuidhinisha ada ya mwaka ya wakurugenzi wasio watendaji ya dola za Kimarekani 482 000 kwa mwaka | | | |

Imetiwa sahihi tarehe | mwezi | Agosti 2025

Sahihi: | Sahihi:

**Fomu ya mwakilishi iliyojazwa iwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni ya Vodacom Tanzania PLC kabla saa 4 asubuhi, Ijumaa tarehe 15 Agosti 2025.**

# **Maelekezo ya** fomu ya mwakilishi

1. Mwanahisa anayepaswa kuhudhuria katika mkutano mkuu anaweza kuteua mwakilishi wake kuhudhuria, kutoa maoni na kupiga kura kwa niaba yake. Mwakilishi sio lazima awe mwanahisa wa kampuni. Kwa makampuni, fomu ya mwakilishi ijazwe na afisa mwenye mamlaka na iwekwe muhuri wa Kampuni husika.
2. Weka alama 'X' kwenye eneo la kujaza kwenye fomu kulingana na kura unayotaka kupiga katika agenda husika. Iwapo utapenda kupiga kura kwa hisa pungufu ya hisa unazomiliki, onyesha idadi ya hisa pungufu ambazo ungependa zipige kura. Iwapo maelekezo haya hayatazingatiwa, mwakilishi atapiga kura atakavyoona inafaa.
3. Mwanahisa anaweza kuweka jina la mwakilishi/wawakilishi wake kwenye sehemu iliyoonyeshwa kwenye hii fomu bila kufuta kipengele cha kuwakilishwa na "Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa mwaka" kilichopo chini ya sehemu ya kuandika majina ya wawakilishi. Mwanahisa atapaswa kuweka sahihi yake iwapo atafuta kipengele hicho. Mwakilishi ambaye jina lake limejazwa likiwa la kwanza kwenye fomu ya uwakilishi akihudhuria mkutano mkuu ndiye atahusika kufanya maamuzi.
4. Fomu za mwakilishi zilizojazwa pamoja na hati ya hisa au risiti ya uwekezaji ya DSE ya mwanahisa, ziwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni – ghorofa ya 15, Vodacom Tower, Ursino Estate, Kiwanja na 23, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanzania kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa tarehe 15 Agosti 2025. Aidha, fomu zinaweza kusainiwa kisha kuzituma kwa barua pepe ya **investorrelations@vodacom.co.tz**.
5. Mwanahisa akifanya masahihisho/mabadiliko yoyote kwenye fomu ya mwakilishi, atapaswa kuwekwa sahihi yake pembeni ya masahihisho/mabadiliko hayo.
6. Wenye hisa wenye umri mdogo kisheria wanapaswa kusimamiwa na wazazi/walezi wao ambao watapaswa kuwa na nyaraka za kisheria za kuwathibitisha.
7. Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa mwaka atakubali fomu ya mwakilishi itakavyokuwa imejazwa tofauti na matakwa haya iwapo ataridhika na namna ambavyo mwanahisa atapenda kupiga kura.
8. Kwa wale wenye hisa za pamoja/vikundi:
   - Yeyote kati yao anaweza kutia sahihi kwenye fomu hii
   - Kura ya mwanahisa mkubwa (ukubwa wa hisa utajulikana kulingana na majina yaliorodheshwa kwenye rejista ya wanahisa wa Kampuni) itakayopigwa na yeye binafsi au kutumia mwakilishi, ndio itakayoruhusiwa kwa niaba ya wanahisa wenzake kwenye kikundi.

**Bi Caroline Mduma**
Katibu wa Kampuni

Ghorofa ya 15, Vodacom Tower, Ursino Estate,
Kiwanja na 23, Barabara ya Bagamoyo,
P.O. Box 2369,
Dar es Salaam
Barua pepe: investorrelations@vodacom.co.tz

# **Taarifa kuhusu** umiliki

| Jumla ya hisa | # ya hisa | % ya hisa |
|---|---|---|
| Kundi la Makampuni ya Vodacom (Vodacom Group Limited) | 1 680 000 200 | 75.0% |
| Mfuko wa Pensheni wa Wafanyakazi wa Serikali (Uwekezaji wa Shirika la Umma SOC Limited, Jamhuri ya Afrika Kusini) | 164 503 540 | 7.3% |
| Wawekezaji wa Kitaasisi (Afrika Mashariki) | 255 008 152 | 11.4% |
| Wawekezaji wa Kitaasisi (Sehemu nyingine duniani) | 46 356 052 | 2.1% |
| Wawekezaji wengine | 94 132 356 | 4.2% |
| | **2 240 000 300** | **100.0%** |

| Umiliki wa hisa kitaasisi | % Umiliki kitaasisi |
|---|---|
| Tanzania | 48.8% |
| PIC | 35.3% |
| Uganda | 6.0% |
| Wanahisa wengine wa kimataifa | 9.9% |
| | **100.0%** |



# Taarifa za kampuni

**Vodacom Tanzania Public Limited Company**
(Imeandikishwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
Usajili namba: 38501
(ISIN: TZ1996102715 Share Code: VODA)

## Wakurugenzi

**D Tarimo (Mwenyekiti)[1]**
**P Besiimire (Mkurugenzi Mtendaji)[2]**
**H Bujiku (Mkurugenzi wa Fedha)[3]**
**K Mutooni[4]**
**M Ikongo [3]**
**M Mbungela[5]**
**N Nyoka[5]**
**R Morathi[5]**
**H Ammar[6]**
**M Abdallah[6]**
**D Kastelic[7]**
**T Semane[5]**

1.Muingereza 2.Mganda 3.Mtanzania 4.Mkenya 5.Mwafrika Kusini 6.Mmisri 7.Mslovak

## Katibu wa Kampuni

**Caroline Mduma**
Ghorofa ya 15, Vodacom Tower,
Eneo la Ursino, Kiwanja namba 23
Barabara ya Bagamoyo
S.L.P 2369
Dar es Salaam, Tanzania

## Ofisi iliyosajiliwa

Ghorofa ya 15, Vodacom Tower
Eneo la Ursino, Kiwanja namba 23
Barabara ya Bagamoyo
S.L.P 2369
Dar es Salaam, Tanzania

## Mkaguzi wa Hesabu za Fedha

**Ernst & Young Inc.**
EY House, Kiwanja namba 162/
1 Barabara ya Mzinga
14111 Oysterbay
S.L.P 2475
Dar es Salaam, Tanzania

## Washauri wa Mambo ya Kisheria

**Dentons EALC East African Law** Chambers
Nyumba namba 18
Mtaa wa Rukwa Masaki
S.L.P 38192
Dar es Salaam, Tanzania

**IMMMA (Advocates)**
Kiwanja namba 357, IMMMA House
Barabara ya Umoja wa Mataifa, Upanga
S.L.P 72484
Dar es Salaam, Tanzania

**Lawhill**
14112 Regent Estate Mikocheni
Mtaa wa Historia, Kiwanja namba 311
Nyumba namba 96
S.L.P 105646
Dar es salaam, Tanzania

## Msajili Masuala ya Hisa

**CSD & Registry Company Limited**
Ghorofa ya 1, Exchange Tower
NHC Morocco Square
S.L.P 70081
Dar es Salaam, Tanzania

**Mshauri Mkuu aliyesajiliwa**
Orbit Securities Company Limited

## Mawasiliano ya nje

***Zuweina Farah***
Mkurugenzi wa Masuala ya Mahusiano na Taasisi ya Vodacom
Ghorofa ya 15, Vodacom Tower
Eneo la Ursino, Kiwanja namba 23
Barabara ya Bagamoyo
S.L.P 2369
Dar es Salaam, Tanzania

## Watoa huduma za Kibenki

**Citibank Tanzania Limited**
Citibank House
Kiwanja namba 1962, Barabara ya Toure, Oysterbay
S.L.P 71625
Dar es Salaam, Tanzania

**National Bank of Commerce Limited**
Barabara ya Sokoine & Mtaa wa Azikiwe
S.L.P 1863
Dar es Salaam, Tanzania

**NMB Bank Plc**
Mtaa wa Ohio /Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P Box 9213
Dar es Salaam, Tanzania

**CRDB Bank Plc.**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 268
Dar es Salaam, Tanzania

**Standard Chartered Bank Tanzania**
Jengo la International House
Mtaa wa Shaaban Robert/Garden Avenue
S.L.P 9011
Dar es Salaam, Tanzania

**Stanbic Bank Tanzania Limited**
Centre Branch
Kona ya Ali Hassan Mwinyi/
Kinondoni Road
S.L.P 72647
Dar es Salaam, Tanzania

**Mahusiano na Wawekezaji**
Albert Maneno
Neema Munuo
Barua pepe: **investorrelations@vodacom.co.tz**
Tovuti: **https://www.vodacom.co.tz/financials**



# Dai la haki

## Taarifa zisizofuata Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha ('IFRS')

Taarifa hii ina baadhi ya hatua zisizofuata Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha ambazo hazijapitiwa au kuripotiwa na wakaguzi wa Kundi la Kampuni za Vodacom ('Kundi'). Menejimenti ya Kundi inaamini hatua hizi zinatoa taarifa muhimu za ziada kwa kuelewa ufanisi wa Kundi la Vodacom au biashara za Kundi la Vodacom kwa sababu zinaeleza hatua zilizotumiwa na Kundi la Vodacom kutathimini ufanisi. Hata hivyo, taarifa hizi za ziada zilizowasilishwa hazikufasiliwa kwa njia inayofanana na kampuni zote, ikiwa ni pamoja na zile zilizo katika tasnia ya Kundi la Vodacom. Hivyo, inawezekana haiwezi kulinganishwa na hatua zinazofanana na kutolewa taarifa na kampuni nyingine. Kwa kuongezea, ingawa hatua hizi ni muhimu katika usimamizi wa biashara, hazipaswi kuangaliwa kipwekepweke au kama mbadala, badala yake ziwe kama kijalizo, katika hatua za Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha. Rejea katika sehemu ya 'Ufanisi wetu' ya taarifa hii kwa maelezo yanayohusiana na mapato ya huduma, EBIT na mapato kwa kila hisa.

## Alama za biashara

Vodafone, logo ya Vodafone, M-Pesa, Vodacom, Wakulima Waliounganishwa na Vodafone Supernet ni alama za biashara za Vodafone Group Plc (au ina program zinazosubiria). M-Fundi, M-Shamba, M-Pawa na Vodacom Faraja ni alama za biashara za Vodacom Tanzania Public Limited Company (au ina program zinazosubiria). Bidhaa zingine na majina ya kampuni yaliyotajwa hapa yanaweza kuwa alama za biashara za wamiliki wao husika.

## Matamko ya matarajio

Taarifa hii, ambayo inajumuisha matokeo ya Kundi la makampuni kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2025, ina 'matamko ya matumaini', ambayo hayajapitiwa au kuripotiwa na wakaguzi wa Kundi, kuhusiana na hali ya kifedha ya Kundi, matokeo ya uendeshaji na biashara na taarifa zinazohusiana na mipango na malengo ya Kundi la Vodacom. Hasa, matamko hayo ya kuangalia mbele yanajumuisha matamko yanayohusiana na: ufanisi wa baadaye wa Kundi la Vodacom; matumizi ya mtaji siku zijazo, ununuzi, kujitoa, gharama, mapato, masharti ya kifedha, sera ya gawio na maendeleo ya baadaye; mikakati ya biashara na uwekezaji inayohusiana na upanuzi na ukuaji wa Kundi la Vodacom; athari za udhibiti wa biashara za Kundi la Vodacom unaofanywa na serikali katika nchi inapofanya shughuli zake; matarajio ya Kundi la Vodacom kuhusiana na tarehe za uzinduzi na kuanza uuzaji wa bidhaa, huduma au teknolojia; matarajio kuhusu mazingira ya uendeshaji na hali ya soko; ongezeko la wateja na matumizi; na kiwango cha ongezeko la gawio kwa Kundi.

Matamko ya kuangalia mbele wakati mwingine, lakini si wakati wote, hubainishwa kwa matumizi yao ya tarehe katika wakati ujao au Maneno kama 'nita', 'tarajia', 'kusudia', 'ninge', 'weza', 'paswa', 'amini', 'panga' au 'lenga' (pamoja na miundo yao ya ukanushi).

Kwa hali yao, matamko ya kuangalia mbele kwa asili yanatabirika, yanaweza kukisiwa na yanajumuisha hatari na mashaka kwa sababu yanahusiana na matumio na yanategemea mazingira ambayo yanaweza kutokea au yasitokee siku za baadaye. Kuna sababu mbalimbali ambazo zinaweza kusababisha matokeo halisi na maendeleo kutofautiana kabisa kuanzia yale yaliyoelezwa au kumaanishwa na matamko haya ya kuangalia mbele. Sababu hizi ni pamoja na, ingawa haziishii hapo, zifuatazo: mabadiliko katika hali ya kiuchumi au kisiasa katika masoko yanayohudumiwa kwa shughuli za Kundi la Vodacom; ushindani mkubwa kuliko ilivyotarajiwa; gharama kubwa kuliko ilivyotarajiwa au matumizi ya mtaji; ongezeko dogo la wateja kuliko ilivyotarajiwa au kupungua kwa wateja wa kudumu; mabadiliko katika hali ya matumizi ya wateja wapya wa waliopo; uwezo wa Kundi kupanua nafasi yake kimawanda au kuongeza muda au kuchukua leseni mpya; uwezo wa Kundi kufanikisha kuokoa gharama; uwezo wa Kundi kutekeleza mkakati wake wa kutumia mkongo; kuanza kutoa bidhaa na huduma mpya; huduma za data (mobile data), upanuzi wa Biashara na mtandao wa 4G, mabadiliko katika viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, na vilevile katika viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, na vilevile viwango vya riba; uwezo wa Kundi kupata faida kutokana na kuingia katika ubia au kufanya biashara pamoja na kuingia katika kufanya biashara ya huduma na utoaji wa leseni ya chapa; matokeo yasiyofaa kwa Kundi ya kufanya na kuchanganya ununuzi na utupaji; mabadiliko katika mfumo wa kisheria ambapo Kundi huendesha shughuli zake; athari za mashauri ya kisheria na mengineyo; kupoteza wasambazaji au kuvurugika kwa mnyororo wa usambazaji; maendeleo katika hali ya fedha ya Kundi, mapato na fedha zinazosambazwa na mambo mengine ambayo Bodi imezingatia wakati wa kuamua viwango vya magawio; uwezo wa Kundi kuwa na mtaji wa kufanyia kazi na mahitaji mengine; mabadiliko katika viwango vya kodi kisheria au mchanganyiko wa faida; na/au mabadiliko katika sharia ya kodi. Matamko mengine yote yaliyofuata ya kuangalia mbele yawe kwa maandishi au mdomo ambayo ni ya Kampuni, kwa mhusika yeyote wa Kundi au kwa watu wowote wanaofanya kwa niaba yao wanastahili katika wingi wao kwa sababu zinarejelewa hapo juu. Uhakika hauwezi kutolewa kuwa matamko ya kuangalia mbele katika waraka huu yatafikiwa. Kutegemea kufuata sharia na kanuni zinazotumika, Kampuni haikusudii kuboresha matamko haya ya kuangalia mbele na haichukui wajibu wowote wa kufanya hivyo.